epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Februari 5, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581943
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
**MAN CITY YAMTWAA RASMI GONZALEZ**


UKURASA WA 3
**Wizi** sigara, vocha dukani wawapeleka jela miaka 42

UKURASA WA 5
**CCM** yaanika vigezo, masharti uteuzi wagombea udiwani, ubunge

UKURASA WA 8
**Wabunge** waibana PSSSF kwa kutoza michango wastaafu

# Watu 900 wauawa mapigano ya DRC

• **M23** yasitisha mashambulizi; EAC, SADC kukutana Dar wiki hii... *Endelea ukurasa 19*



Ruto

Kagame

Tshisekedi

## Yaliyombeba Samia sekta ya afya hadi kutunukiwa tuzo



UKURASA 2



UKURASA 4

RIPOTI MAALUM

## Ulivyo mtihani usafi vyoo vya Kituo cha Mabasi cha Magufuli



**MICHEZO** **FADLU: SIMBA UGENINI KAMA NYUMBANI** UK.24

**KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

## Kamati ya Bunge yabaini upigaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imebaini Sh. milioni 937.3 za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) zilizokopeshwa hazijarejeshwa hali inayoathiri utoaji wa mikopo kwa wanawake kufikia tija iliyokusudiwa.

Akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo jana bungeni, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alisema mfuko huo ulianzishwa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya uendeshaji wa miradi ya kiuchumi wanawake kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu.

Alisema mfuko huo una mtaji wa kiasi cha Sh.bilioni 1.27 na kati ya fedha hizo zilizopo kwenye akaunti ni Sh.milioni 322. 5.

"Kiasi cha Sh. 475,488,459.90 ni madeni yalipo halmashauri ambayo hayajarejeshwa na Sh. 461,825,598 ni madeni ambayo wizara ilivikopesha vikundi vya wajasiriamali na mjasiriamali mmoja mmoja,"alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kamati imebaini kuwa kumekuwa na urejeshwaji usioridhisha kutoka halmashauri na vikundi vilivyokopeshwa hivyo kufanya mfuko kuwa na madeni ya muda mrefu na kupelekea kushindwa kutoa mikopo kwa walengwa.

"Kwa kuwa kumekuwa na mikopo ya muda mrefu iliyokopeshwa kwa halmashauri, wanawake na vikundi mbalimbali nchini na haijarejeshwa na kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunaathiri utolewaji wa mikopo kwa wanawake wengine wenye vigezo vya kupata mikopo hiyo na hivyo kuathiri nia njema ya serikali ya kuwainua wanawake kiuchumi," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema Bunge limeazimia serikali iweke mkakati unaotekelezeka wa kuhakikisha fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa na kutumika kama ilivyokusudiwa.




Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), John Mnali (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu mkutano wa biashara baina ya Tanzania na Italia unaotarajiwa kufanyika Februari 11 na 12. Kushoto ni Balozi wa Italia nchini, Giuseppe Coppola na Claudio Pasqualucci kutoka Taasisi ya ICE. **Habari Uk. 8**. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Yaliyombeba Samia sekta ya afya

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepokea tuzo ya heshima ya 'The Gates Goalkeepers Award' kutambua juhudi zake za kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa asilimia 80, kuboresha upatikanaji huduma za afya na kukuza usawa wa kijinsia katika sekta hiyo.

Kiongozi huyo anakuwa wa saba duniani na wa kwanza Afrika kutunukiwa tuzo hiyo ambayo hutolewa kwa viongozi waliowezesha nchi zao kuharakisha maendeleo kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Kutokana na tuzo hiyo iliyotolewa na Taasisi ya The Gates Foundation, Rais Samia katika hotuba yake jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, aliainisha maendeleo ya nchi katika kuboresha huduma za afya na lishe na kusisitiza umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika mifumo inayozingatia utu wa kila mtu.

Rais Samia alitoa tuzo hiyo kwa wafanyakazi wa sekta ya afya kama njia ya kukubali kujitolea kwao bila kuchoka na kuainisha maeneo kadhaa yaliyochangia nchi kuipata na kazi inazoendelea kufanya.

"Tuzo hii ni ya kutia moyo kwa sababu nyingi, hasa Gates Foundation, pamoja na kuwa mdau muhimu katika ajenda ya kimataifa ya afya, imeendelea kuwa mshirika muhimu wa Tanzania," alisema.

Rais Samia alisema tuzo hiyo ni utambuzi wa uongozi wa pamoja na dhamira ya watanzania wanaofanya kazi bila kuchoka kuboresha maisha ya wanawake, watoto na familia na kusisitiza uboreshaji lishe umekuwa msingi wa ajenda ya nchi kwa maendeleo ya taifa.

Rais Samia alieleza namna nchi ilivyowekeza katika afya ya uzazi, uwekezaji kwenye vituo vya afya na watumishi na kutoa kipaumbele kwa afya ya mama na mtoto.

"Tangu mwaka 2021 (alipoingia madarakani), tumechukua hatua mbalimbali za kuboresha afya ya uzazi, mtoto mchanga na vijana wanaobalehe pamoja na lishe.

"Inatia moyo kuona kwamba kutokana na afua mbalimbali za kimkakati, uwiano wa vifo vya uzazi umepungua kama inavyosemwa hapa. Lakini pia, vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka asilimia 67 hadi asilimia 43 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa, ni matokeo ya juhudi za pamoja," alisema.

Rais Samia alisema wameongeza idadi ya madaktari bingwa waliosajiliwa kutoka 69 mwaka 2020 hadi 338 mwaka 2024.

"Tumekuwa tukitoa huduma za afya za uzazi bila malipo na kwa watoto chini ya miaka mitano. Pia tumeimarisha mifumo ya rufani kwa kuongeza magari 727 ya wagonjwa katika kipindi cha miaka tisa kuanzia 2015 hadi 2024 na hivyo kuimarisha upatikanaji huduma za dharura za uzazi kwa kuziba pengo kati ya jamii za vijijini na vituo vya afya," alisema.

Rais Samia alisema wameanzisha pia huduma za rufani za dharura za mama na mtoto aliyezaliwa na kuongeza idadi ya mashine za ultrasound kutoka 345 mwaka 2020 hadi 970 mwaka 2024.

Pia alizungumzia ujenzi mkubwa wa barabara za vijijini ili kurahisisha safari za kwenda na kurudi kwenye vituo vya afya.

"Nne, tumesaidia katika kuendeleza TEHAMA ili kufanya tathmini ya vifo vya kinamama wajawazito na matokeo yake ni kutambua uwezo wa kudhibiti baadhi ya matatizo ya uzazi na imeongeza juhudi za kuimarisha kujenga uwezo kupitia ushauri kwa watoa huduma za afya.

"Tano, serikali ilianzisha mikakati ya kisekta, ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia, tathmini ya lishe kwa kununua mashine ambazo zimeimarisha uwezo wa taifa kufanya uchambuzi unaohusiana na lishe, kama vile matumizi ya sampuli za kibaolojia ili kupata hali ya lishe kwa kutumia utaalamu wa ndani.

"Udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 42 mwaka 2015 hadi asilimia 30 na uzito mdogo umepungua kutoka asilimia 16 hadi asilimia 12 katika kipindi hichohicho," alisema.

Rais Samia alisema bado wanaendelea kuchukua hatua zinazohitajika ili kupunguza uzito mdogo, udumavu na utapiamlo.

Mkuu wa Nchi pia aliangazia juhudi zinazoendelea za kushughulikia afya ya vijana, hasa kwa kuzingatia kuzuia mimba za utotoni kunakolenga kukabiliana na vikwazo vya kitamaduni na kimila, ili kuhakikisha maisha ya baadaye ya afya kwa vijana wa taifa hilo. Alisema matokeo ya juhudi hizo, mimba za utotoni zimepungua kutoka asilimia 27 hadi asilimia 22.

"Sita, kupelekwa kwa wafanyakazi wa afya ya jamii ambao wamekuwa muhimu wanaohakikisha kunakuwa na upatikanaji huduma muhimu za afya katika ngazi ya chini na kuwa kiungo muhimu kati ya vituo vya afya na jamii kutoa elimu muhimu ya afya na kukuza chanjo na lishe programu," alisema.

Alisema wamechangia katika ongezeko la ufahamu na kushughulikia vikwazo kama vile mila na desturi za kitamaduni.

"Bado tuna kazi ya kufanya ili kuboresha zaidi huduma za afya, zaidi ya hayo, changamoto zingine kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, milipuko ya kikanda na ukosefu wa usawa wa kiuchumi zinatukumbusha kwamba kazi yetu lazima iendelee kwa nguvu mpya," alisema.

Rais wa Usawa wa Kijinsia kutoka Taasisi ya Gates Foundation, Anita Zaidi alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika afya ya mama na mtoto katika miaka kadhaa iliyopita.

"Kupitia mifumo iliyoimarishwa ya huduma za afya, kuboreshwa kwa upatikanaji huduma za uzazi na kuzingatia matunzo bora, kinamama wengi zaidi wananusurika wakati wa kujifungua na watoto wengi zaidi kuwa na fursa ya kustawi," alisema.

Anita alibainisha kuwa dhamira ya Tanzania katika SDG, ambayo ilitia saini mwaka 2015, imeiweka kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine.

"Kuanzishwa kwa mipango kama vile programu ya M-MAMA, ambayo inahakikisha wajawazito wanapata usafiri wa dharura hadi kwenye vituo vya afya, ni mfano mmoja wa mbinu za maendeleo ya nchi," alisema.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alisema tuzo hiyo ni uthibitisho wa uongozi wa kipekee wa Rais Samia na dhamira isiyoyumba katika kuboresha huduma za afya.

**APOKEWA DODOMA**

Muda mfupi baada ya kupokea tuzo hiyo, Rais Samia alikwenda Makao Makuu ya Nchi jijini Dodoma, alikopokewa na viongozi wa serikali na chama na kuwaeleza kuwa dunia imetambua jitihada za serikali katika huduma za afya hasa kwa kinamama.

Alikumbushia kuwa miaka minne iliyopita vifo vilivyotokea wakati wa kujifungua vilikuwa 556 kati ya wajawazito 100,000 waliofika hospitalini kupata huduma ya uzazi.

"Lakini kwa sababu tumefanya uwekezaji mkubwa kwenye afya, kwa kujenga majengo mengi, upatikanaji vifaa tiba na kusomesha wafanyakazi, tumepunguza vifo kutoka 556 mpaka 104 kati ya wajawazito na malengo ya dunia ifikapo mwaka 2030 tuwe na vifo 70 tu na tunaamini tutafika huko na tutavuka lengo.

"Lakini kwa watoto chini ya miaka mitano tumepunguza vifo japo tuna kazi kubwa ya kufanya kwa wanaozaliwa, tulikuwa tunawapoteza kwa mambo kadhaa ikiwamo matumizi ya dawa za kienyeji, kuchelewa kufika hospitalini pamoja na kukosa vifaa vya kuokoa maisha yao," alisema Rais Samia.

***Taarifa za ziada: Halfani Chusi***

***Kwa maoni; +255 677 020 701***
***Email; costumerrelations@guardian.co.tz***

## HABARI KITAIFA

# Bunge lataka uendelezaji mfuko wa UKIMWI kuepuka utegemezi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeazimia serikali kutekeleza kikamilifu mpango wa uendelevu wa mwitikio wa Virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI nchini, ili kuondokana na utegemezi wa msaada kutoka kwa wafadhili.

Akiwasilisha jana bungeni taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Elibariki Kingu, alisema kiwango kikubwa cha utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI nchini hutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

Alisema ufadhili huo ukifikia ukomo unaweza kusababisha kwa kiasi kikubwa nchi kupunguza kasi ya kupambana na janga hilo kwa kukosa fedha za kutosha.

Pia alisema Bunge liazimie serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sheria ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe na Viungo vya Mwili wa Binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hiyo kwa kulinda haki za binadamu na kuzuia biashara haramu ya viungo vya mwili wa binadamu.

Kingu alisema huduma za uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu hazina sheria rasmi.

Alisema kufanyika kwa huduma hizo bila uwapo wa sheria rasmi kunaweza kusababisha athari hasi kwa jamii, ikiwa ni pamoja na kukiukwa kwa haki za binadamu na kuibuka kwa biashara haramu ya viungo vya binadamu.

Kuhusu Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHC), Kingu alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, kamati imebainisha vyanzo vya fedha za kugharamia wasio na uwezo kupitia sheria hiyo ambavyo vilitarajiwa kukusanya Sh.bilioni 173.5 na hadi kufikia Novemba 23, 2024, kiwango kilichokusanywa ni Sh. bilioni 47.13 sawa na asilimia 27.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakiwa wamebeba mwili wa mmoja kati ya wachimbaji wadogo watatu walioangukiwa na kifusi wakati wakichimba madini katika mgodi wa Nkandi, mtaa wa Ilindi-Mwine, kata ya Zongomela, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wakati wa zoezi la uokoaji, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wizi vocha, simu wawapeleka jela miaka 42

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

WATU wanne wamehukumiwa kifungo cha maka 42 gerezani baada ya kupatikana na hatia katika kesi namba 5,537 ya mwaka 2024 ya kuvunja duka na wizi wa sigara, vocha na simu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Tunduru, Shughuli Mwampashe baada ya kujiridhisha bila shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri katika shauri hilo.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mwampashe alisema mshtakiwa namba tatu na namba nne wanahukumiwa kifungo cha miaka 24 gerezani na mshtakiwa na namba mbili anahukumiwa kifungo cha miaka 18 gerezani baada ya kusikiliza ombi lao.

Waliohukumiwa kutumikia adhabu hiyo ni Sophia Mtewa aliyekutwa na hatia ya kuwapokea washtakiwa na kuwaficha nyumbani kwake wakati wakitekeleza uhalifu huo.

Wengine ni Hamis Mchivali, Mfaume Namangwalu na Salum Hassan aliyewahifadhi nyumbani kwake ili wasikutane na mkono wa sheria licha ya kufahamu kuwa ni wahalifu.

Washtakiwa watatu walikuwa wanakabiliwa na mashtaka manane, mmoja akikabiliwa na shtaka moja. Shtaka la kwanza na la tatu ni kwa mshitakiwa namba mbili na tatu kwa kosa la kuvunja jengo na wizi kinyume cha kifungu cha 299(a) na (b) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

Ilidaiwa mahakamani huko na Mwendesha Mashtaka, Inspekta Ernest Machiya kwamba Agosti 6, 2024, katika kijiji cha Cheleweni, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, washtakiwa walivunja na kuingia katika duka la Mussa Mpanjikwa kwa nia ya kutenda kosa la wizi.

Alidai kuwa mara baada ya kuvunja na kuingia katika duka hilo, washtakiwa hao waliiba simu janja moja aina ya Sumsang Galaxy A3 yenye thamani ya Sh. 534,000, mali ya Mussa Mpanji

Katika shtaka la tatu, washtakiwa walidaiwa kuvunja na kuingia katika duka la Yona Mligo kwa nia ya kutenda kosa la wizi, huku katika shtaka la nne, kwa pamoja walidaiwa kuvunja, kuingia na kuiba simu mbili, moja aina ya TECNO T 301 yenye thamani ya Sh. 30,000 na nyingine aina ya Oking yenye thamani ya Sh. 30,000, mali ya Yona Mligo.

Kwa mujibu wa Inspekta Machiya, katika shtaka la tano, mara baada ya kuvunja na kuingia ndani ya duka, washtakiwa waliiba simu aina ya Tecno T 528, mali ya Seleman Hassan yenye thamani ya Sh. 50,000 katika duka la Yona Mligo.

Katika shtaka la sita, walidaiwa kuvunja na kuingia ndani ya duka na kuiba simu moja aina ya Tecno Pop 5 yenye thamani ya Sh. 180,000, mali ya Hamis Tawakali.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa katika kosa la saba na la nane, mshtakiwa namba nne alipatikana na mali isiyo halali kinyume cha kifungu cha 312(1)(b) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16 Agosti 7, 2024 katika kitongoji cha Kigamboni, wilayani Tunduru.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa washtakiwa hao walipatikana na pakti 13 za sigara aina ya Winston zenye thamani ya Sh. 39,000, pia pakti saba zingine za Winston za rangi nyekundu zenye thamani ya Sh. 21,000, pakti moja ya sigara aina ya Sports yenye thamani ya Sh. 5,000, pakti 10 za sigara aina ya Master Menthol za Sh. 30,000, pakti 19 za sigara aina ya Master Filter zenye thamani ya Sh. 57,000.

Washtakiwa hao pia walidaiwa kukutwa na pakti sita za sigara aina ya Clessent na Star, zote zina thamani ya 170,000.

Katika shtaka la nane, washtakiwa walidaiwa kukutwa na mali isiyo halali; vocha za mitandao ya simu tofauti, vocha 35 za Vodacom za Sh. 500, vocha 60 za TTCL za Sh. 500, vocha 66 za Halotel za Sh. 500 na vocha 53 za Airtel za 500, zote zikiwa na thamani Sh. 107,000.

Mshtakiwa namba moja alidaiwa kushirikiana na wahalifu kwa kuwahifadhi kinyume cha sheria, akikiuka kifungu cha 388 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

"Mnamo Agosti 6, 2024, mshtakiwa namba moja kwa jina Sophia Rajabu Mtewa, aliwapokea washtakiwa Hamis Mchivali, maarufu Chake, Mfaume Mussa Namangwalu na Salum Said Hassan, maarufu kama Kanda, akiwa na ufahamu kwamba ni wahalifu na kuwahifadhi ili wasikutane na mkono wa sheria," alidai.



KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI

# Ulivyo mtihani wa usafi vyooni kuanzia abiria hadi walio kazini



Mwonekano wa nje wa vyoo vya wanawake katika stendi hiyo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**Na Christina Mwakangale**

LICHA ya kulipia huduma, maelfu ya abiria wanaotumia Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, mkoani Dar es Salaam, wako hatarini kupata magonjwa, yakiwamo maambukizi katika mfumo wa mkojo (UTI), kutokana na vyoo vya stendi hiyo kuwa kwenye mazingira machafu.

Stendi ya Magufuli ni moja ya vituo bora vya mabasi nchini na Afrika Mashariki. Ujenzi wake uligharimu Sh. bilioni 50, ina matundu 140 ya vyoo. Kati yake, 56 ni kwa ajili ya wanaume.

Hata hivyo, ni jambo la kawaida kukuta maji yametuama kwenye sakafu za vyoo vya stendi hiyo. Hali ni mbaya zaidi upande wa vyoo vya wanawake, ambavyo havina vyombo maalum vya kutupa taka ngumu, zikiwamo taulo za kike, ndoo za kuhifadhia maji zimechakaa na makopo yanayotumika ni dumu la lita tano, ambalo limekatwa.

Kituo hicho, kama ilivyotolewa ufafanuzi na uongozi wake, kinahudumia wastani wa abiria 16,000 hadi 20,000 kwa siku. Hao ni mbali na wanaokwenda kusindikiza au kuwapokea ndugu zao, wafanyakazi wa mabasi na wafanyabiashara ndogo.

Watumiaji hao wa kituo hicho wanatakiwa kulipa ushuru wa aina mbili; kwanza Sh. 300 ya kiingilio cha getini kwa wale ambao hawana tiketi za mabasi na Sh. 200 kwa kila anayehitaji kwenda msalani kujisaidia.

Mbali na abiria na wasindikizaji wao, pia kuna makundi mengine ya watumiaji huduma za msalani kituoni huko ni vibarua wasukuma matoroli ya kubeba mizigo, wajasiriamali wadogo ambao kwa pamoja wanafikia 360.

Doreen Mwakabuta, ambaye anajitambulisha ni msafiri wa mara kwa mara anayetumia kituo hicho kwenda mikoa tofauti nchini, anasema kila anapofika kituoni huko, hulazimika kuwa na tafakuri ya muda kuingia msalani, akihofia kupata magonjwa kama vile UTI.

"Unajua kwa wanawake, magonjwa ya mfumo wa mkojo ni rahisi kuambukizwa iwapo choo si safi. Binafsi nikiingia katika choo chenye majimaji yaliyosambaa sakafuni, kinatoa harufu, huwa ninakosa raha, nitajisaidia kwa shida," anasema.

Doreen ana lingine la ziada -- vyoo hivyo si rafiki kwa matumizi ya watu wenye ulemavu. Ujenzi wake haukuzingatia mahitaji ya kundi hilo.

Dereva wa basi linalofanya safari kati ya Dar es Salaam na Songea, Ayubu Mambosasa, anasema kampuni anayofanyia kazi, ina ofisi nje ya kituo hicho cha mabasi, hivyo ni mara chache huingia kutumia vyoo vya stendi hiyo.

"Ninaingia chooni mara chache, labda nibanwe sana kwa sababu ninajua kitu chenye matumizi mengi, lazima kina changamoto. Usafi ni mdogo, ila nikibanwa ninaingia, sina namna," anasema dereva huyo.

Geofrey Godson ni msukuma toroli anayesaidia abiria kubeba mizigo yao katika stendi hiyo. Anasema amefanya kazi hiyo kwa miaka miwili, kazi anayoitaja inamwezesha kuendesha maisha yake.

"Huduma ya choo ni Sh. 200 kila unapohitaji huduma. Na kwetu sisi ambao tuko chini ya kampuni tunavaa sare, lakini tunalipia isipokuwa getini tu ndiko hatulipii kwa sababu tuna hizi sare. Kuna wakati huwa ninajibana nisinywe maji mengi, ili nisiende msalani mara nyingi.

"Lakini kwa kuwa sisi ni wanaume, unaweza kwenda sehemu ukajibanza kujisaidia haja ndogo hata katika chupa ya maji, unaiacha hapo hapo. Fedha ninayopata kwa siku haizidi Sh. 20,000, hapo kuna Sh. 11,000 ya bosi, ninywe chai, chakula mchana na usiku," Godson anasimulia.

Amina Shaban, mchuuzi katika kituo hicho kwa miaka mitatu sasa, akiuza bidhaa ndogo kama karanga, pipi, biskuti, maji na juisi, anasema kuwa kila siku anapoingia getini alfajiri hulipia Sh. 300 na anapoingia msalani hulipia Sh. 200.

"Hiyo Sh. 200 unalipa kila unapoingia msalani. Pale tumbo linapovurugika ndipo gharama inakuwa kubwa zaidi na biashara ni ya kawaida si nzuri, faida ni ndogo bado, sijala, sijanywa maji. Inabidi kuwa makini na unywaji wako wa maji.

"Hata ukibanwa inabidi ujibane kidogo. Kwa ujumla kama unashinda humu, suala la maji ya kunywa hatulipi kipaumbele. Kwa sababu chai asubuhi si chini ya Sh. 1,000, chakula cha mchana labda Sh. 1,500, bado usiku urudi nyumbani ukapike, biashara yenyewe iko wapi?" Amina anahoji.

Wakati baadhi ya wachuuzi katika Stendi ya Magufuli wakijizuia kunywa maji kwa hofu ya gharama za ushuru wa huduma ya choo, Bingwa wa Magonjwa ya Figo na Mfumo wa Mkojo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Jonathan Mngumi, anaonya kuwa mtu yeyote anayefanya kazi nzito juani au inayomfanya atokwe jasho jingi, ana kiwango maalum cha unywaji maji.

"Kwa wastani mtu mzima anayefanya kazi nzito juani au kazi ya kutoka jasho jingi, anashauriwa kunywa maji kati ya lita tatu hadi tano kwa siku kulingana na kiwango cha jasho na unyevunyevu wa mazingira.

"Kujinyima kunywa maji na uko kwenye mazingira hayo si sahihi. Kila baada ya saa moja ya kufanya kazi nzito, kunywa takriban mililita 500 mpaka lita moja ya maji.

"Ikiwa mtu anajisikia kiu sana au mkojo wake ni wa rangi ya njano iliyokolea, ni dalili ya upungufu wa maji mwilini na anapaswa kuongeza unywaji maji. Athari za unywaji maji usio sahihi ni pamoja na kuathiri viungo kadhaa muhimu; figo kushindwa kufanya kazi ipasavyo na hata kukumbwa na UTI, ngozi kuwa kavu na kuzeeka haraka.

"Vilevile, moyo huongeza mzigo kwa sababu ya kupungua kwa ujazo wa damu, ubongo unaweza kusababisha maumivu ya kichwa, kutoelewa vizuri na uchovu.

"Unywaji duni wa maji pia husababisha mmeng'enyo wa chakula kuwa duni, husababisha kufunga haja kubwa na kuongeza asidi tumboni, jambo linaloweza kusababisha vidonda vya tumbo," bingwa huyo anatoa tahadhari.

Dk. Mngumi ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Figo na Bingwa wa Magonjwa ya Figo MNH, anasema kwa wastani mtu hujisaidia haja ndogo mara nne hadi saba ndani ya saa 12 hadi 24, sawa na wastani wa kupata haja hiyo kila baada ya saa tatu hadi nne.

"Unywaji duni wa maji huathiri mfumo wa mkojo kuanzia kwenye figo hadi kibofu, huongeza uwezekano wa maambukizi ya UTI, hasa kwa wanawake. Hupunguza uwezo wa kibofu kufanya kazi ipasavyo, jambo linalosababisha hisia ya haja ndogo," bingwa huyo anaonya.

Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (TAKUHA), Solomoni Nkigi, anasema abiria wa makundi yote wana haki ya kupata huduma bora mahali popote, ikiwamo vituo vya abiria.

"Nipashe mmefanya uchunguzi wenu, na sisi tunakwenda kufanya uchunguzi kuhusu vyoo, maana kituo kimejengwa na huduma kama hizi tunaona kama zinakidhi," anasema.

Richard Shumbusho, Mwanasheria kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), anatoa fasili ya huduma ya choo kisheria.

Anasema huduma ya choo ni muhimu kwa sababu inazuia magonjwa, inaboresha usalama na inasaidia maendeleo ya kiuchumi. Hivyo ni jukumu la serikali kulinda haki hiyo, ili kuhakikisha kila mtu anapata huduma bora, safi na salama kwenye maeneo ya mkusanyiko kama stendi hiyo ya mabasi.

"Ni muhimu kuhakikisha kwamba ada hizi (zinazotozwa) hazizuii watu kupata huduma muhimu na kwamba zinatumika kwa ajili ya kuboresha huduma hizo. Serikali inapaswa kuhakikisha kunakuwa na huduma ya choo bora kwa wote bila kujali uwezo wa kifedha wa wahitaji," anasema.

Mwanasheria huyo anasema Ibara ya 138(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inaelekeza ada na ushuru wowote lazima uanzishwe kwa mujibu wa sheria.

"Malipo yanayotozwa kwa huduma za choo, yanapaswa kuwa na msingi wa kisheria, ili kuhakikisha haki za wananchi zinaheshimiwa. Kwa hiyo ada hizi ni muhimu katika kuhakikisha huduma za choo zinapatikana zikiwa salama na zenye ubora kwa watumiaji wote," anasema.

Meneja wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Isaac Kasebo, anasema huduma zinazotolewa kituoni huko kama vile choo zinalipiwa ili kuwa endelevu na bora.

"Changamoto iliyopo kwenye huduma za vyoo ni baadhi ya watumiaji kuharibu miundombinu ya vyoo, jambo linalosababisha upotevu wa maji na matengenezo ya mara kwa mara.

"Jumla ya matundu ya vyoo ni 140 (84 ya wanawake 84) na hufanyiwa usafi muda wote. Maji yanapatikana, tunahifadhi akiba kwenye matangi ya lita 500,000 pia tumejenga kisima kinachotumika pindi maji ya DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam) yanapokatika," meneja huyo anasema.

Kasebo anaeleza kuwa msimu wa mwisho wa mwaka na sikukuu, abiria huongezeka na kufanya kiwango cha mapato pia kuwa juu kutoka wastani wa Sh. milioni nane hadi Sh. milioni 10 kwa siku.

"Vyanzo vya mapato haya ni kutokana na ushuru tofauti, kama vile vyoo, getini, mabasi na pango. Mabasi yanayotoa huduma kwa siku ni kati ya 170 na 200. Wasafiri kwa siku hutegemeana na msimu. Kwa mfano kipindi cha abiria wachache, wanakuwa wa wastani wa abiria 16,831, msimu wa abiria wengi, tunakuwa na wastani wa abiria 20,874," anasema.

*ITAENDELEA KESHO

# Kafulila: Mission 300 imeleta taswira pana uwekezaji nishati

**Na Salome Kitomari**

MKUTANO wa Nishati Afrika (Mission 300) uliofanyika Januari 27 hadi 28, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, umetoa taswira pana kwa sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi ya usambazaji umeme, huku kukiwa na mipango ya kubadili sheria kuruhusu hilo.

Akihojiwa juzi kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na kituo cha ITV, Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), David Kafulila, alisema mtandao wa umeme nchini ni kilomita 8,000 kati yake 2,000 zimejengwa wakati wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, alisema usambazaji hauwezi kufanywa kwa fedha za serikali, hivyo inahitajika mitaji binafsi kwa muundo wa ubia ambao unalazimisha mabadiliko ya sheria kuruhusu hatua hiyo.

Alisema uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme vinahitaji uwekezaji wa serikali na sekta binafsi ili kuwafikia wananchi kwa kuwa kodi au mikopo haiwezi kufanya mambo yote.

"Tunazungumzia megawati 4,000 au 5,000 lakini kwa idadi ya watu inavyoongezeka, mahitaji ya umeme ni makubwa kwa kuzingatia kwamba nchi inataka kujenga uchumi wa pato la dola 4,700 hadi 8,000. Hili linawezekana kwa kukaribisha sekta binafsi kuchangia Dola bilioni tano,.

Tunataka kujenga uchumi mkubwa ambao hauwezi kujengwa kwa kodi na mikopo na kwamba uzoefu unaonesha inahitajika sekta binafsi kuchangia ili serikali ipate nafuu kwa kutofanya kila kitu kwa kodi zake, ili ijielekeze maeneo ambayo sekta binafsi haitavutiwa kuwekeza.

Kwa mujibu wa Kufulila, changamoto hazikosekani lakini hatua kubwa inapigwa kwenye miradi ya maendeleo huku akitolea mfano mradi wa SGR ambao umerahisisha usafiri na kupunguza muda unaopotea barabarani.

"Maendeleo hayapimwi kwa kuangalia ndani, uchumi umebadilika nchi zote zinakopa, Tanzania sio kisiwa lazima tukope lakini deni letu ni himilivu ukilinganisha na nchi za Kusini mwa Afrika na Afrika Mashariki,"alisema.

Kuhusu mikataba rafiki, alisema PPPC itahakikisha ushirikiano ni rafiki kwa pande zote kushirikiana na kwamba mabadiliko ya Sheria ya PPP ambayo yameondoa ugumu kwenye usuluhishi wa migogoro ambayo haikuruhusiwa kwenda kwenye mabaraza ya kimataifa,na kwamba kwa sasa imeruhusu kusuluhisha ndani na nje.

"Si sekta binafsi tu inadhulumiwa, hata serikali inaweza kudhulumiwa na sekta binafsi, serikali inaweza kudhulumiwa ndani na kwenda nje na kushindwa. Uamuzi huu si kwa faida ya mwekezaji pekee bali kwa serikali,"alifafanua.

Mkutano wa Nishati Afrika 'mission 300' uliwaleta pamoja wakuu wa nchi 25, mawaziri na wakuu wa taarifa za fedha Afrika na duniani, huku wote wakitia saini Azimio la Dar es Salaam la kuhakikisha upatikanaji wa Nishati kwa wananchi milioni 300 ifikapo 2030.

Katika mkutano huo, Rais wa AFDB, Dk. Akinwumi Adesina, alisema wao na Benki ya Duania (WB) wametenga Dola za Marekani bilioni 40 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mpango wa awali wa 'Mission 300' wa kufikisha nishati ya umeme kwa wananchi milioni 300 katika nchi za Afrika.

Kati ya fedha hizo, Dola bilioni 22 zitatolewa na WB na Dola bilioni 18.2 zitatolewa na AFDB na kwamba upatikanaji wa umeme ni nyenzo muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ukosefu wa nishati hiyo unapunguza ukuaji wa uchumi kwa asilimia 2.4

Kadhalika, alisema Rais wa Benki ya Kiislamu aliahidi kutoa Dola bilioni 2.6, Rais wa Maendeleo ya Miundombinu akiahidi kutoa Dola bilioni 1.5 na Rais wa Mfuko wa OPEC Dola bilioni moja.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Tanzania ni moja ya nchi 12 zinazotekeleza mpango mahsusi wa taifa kuhusu nishati ambao utaongeza kasi katika kuunganisha umeme nchini hadi kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

Alisema ili kufanikisha mpango huo ndani ya miaka mitano, inahitaji uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni tano zitakazopatikana kutoka katika sekta binafsi.

Pia alisema kupitia mpango huo, Tanzania imejipanga kutekeleza mambo manne ikiwamo kuongeza uzalishaji wa umeme kutokana na nishati mchanganyiko kwamba mpaka sasa ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,431 ambapo asilimia 58 inatokana na vyanzo vya maji,asilimia 35 gesi asilia na asilimia saba kutoka vyanzo vinginevyo.

Rais Samia alisema Tanzania imelenga kuongeza megawati 2,463 za umeme kutokana na jua, gesi asilia, upepo na vyanzo vingine ifikapo mwaka 2030 ambapo kwa sasa inazalisha megawati 1,800, na kwamba mwelekeo wa Tanzania kwa sasa ni kufikisha vitongoji 64,359 na kwamba mpaka sasa imeshavifikia vitongoji 32,827.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wassira, akizungumza katika Kongamano la Umoja wa Wanawake (UWT) kuelekea katika Maadhimisho ya Miaka 48 ya Kuzaliwa CCM, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yaanika vigezo uteuzi wagombea udiwani, ubunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Stephen Wasira, ametaja moja ya vigezo vitakavyotumika kuchuja wagombea wa ubunge na udiwani ndani ya chama kuwa ni kukubalika kwenye jamii yake na si kwa mafurushi ya fedha, vitenge na mitungi ya gesi.

Pia amesema Ilani mpya ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2025 -2030 itakuwa na mambo makubwa ikiwamo kuboresha maisha ya mwananchi mmoja mmoja na kuondoa vikwazo.

Akifungua Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 48 ya CCM lililoandaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Wasira alisema katika mchakato wa kura za maoni, wamekubaliana kuchagua wagombea watatu kwa kila nafasi na moja ya vigezo kitakuwa hicho.

"Kama unagombea UWT tuwe na uhakika kwamba UWT kweli wanakutaka na si kwamba wewe unatembea na mitungi ya gesi, vitenge. Kama unataka kuwapa vitenge si uwape baada ya uchaguzi kuwashukuru? Unawapa vitenge wakuchague sasa watachagua yupi wa vitenge vizuri zaidi au namna gani?" alihoji.

"Lazima kuwa na chama kinachojipambanua kwenye maadili na mimi ndiye msimamizi na Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Maadili namsaidia Rais Samia (Suluhu Hassan). Sasa mimi na maadili tuna uhusiano, mimi nimekua kimaadili," alisema.

Alisema Mwalimu Julius Nyerere (Rais na Mwenyekiti wa Kwanza wa CCM) alijenga chama chenye maadili na si cha kununuana na kuwataka kujitahidi kusafisha chama kwa kuwa kitarithishwa kwa vizazi vijavyo na wasikiue.

Alibainisha kuwa awali mikutano ya kupiga kura za maoni iligeuka kama soko la hisa, watu wanahonga na kwa sasa wigo wa wajumbe umeongezwa ili wasaidie kupata watu wanaokubalika kwenye jamii.

**ILANI MPYA**

Pia alisema kwa sasa wanaandika Ilani mpya ya Uchaguzi ya CCM inayozungumzia maisha ya mtu mmoja mmoja ili kuondoa vikwazo.

"Kwa mfano wakulima tumeanza, Wizara ya Kilimo inapeleka matrekta ya kukodisha kule vijijini ili kuondoa adha ya kutumia jembe la mkono. Kuna mambo makubwa yatakuja katika ilani inayokuja yanayohusu maisha ya watu ndiyo ajenda ya CCM na wakulima wa Tanzania wanaozalisha chakula ni wanawake,"alisema.

Kuhusu mchango wa Rais Samia katika maendeleo ya Tanzania, Wasira alisema Rais John Magufuli alipofariki dunia, watu walikuwa na wasiwasi na kama miradi mikubwa itatekelezwa lakini kwasasa wameshuhudia kazi aliyofanya.

"Sasa wale wanaosema mkutano mkuu kwa nini ulimpitisha Samia jibu lao ni hilo kwamba kazi inaendelea sasa wao wanataka nini? Kama wanaona kazi haiendelei waweke mgombea wao tumwoneshe njia. Njoo na wa kwako ambaye hajajenga hata darasa moja halafu sisi tunakuja na Samia. Huyo wako tutamsindikiza katika kushindwa vibaya,"alisema.

Alisema CCM dhamira yake ni kuboresha maisha ya Watanzania kupitia elimu, afya, kilimo, viwanda, miundombinu na yanafanyika kwa kushika dola kwa njia ya uchaguzi.

Pamoja na hayo, aliwataka wanawake kusimamia suala la malezi kwa vijana wa kike na wakiume na kukemea masuala yanayokwenda kinyume na maadili ya watanzania.

Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema UWT ikiwa imara CCM inakuwa imara na kukielekeza kwenye ushindi.

"Tunasema ushindi wa kishindo kwa sababu kushinda tutashinda, lakini tunataka wa kishindo na hakuna kumpuuza hata sisimizi kila atakayekuja mbele yetu tumchukulie ni mshindani kweli kweli na atakapopata mashambulizi ajue ameshambuliwa na jeshi tunalotegemea ni la wanawake,"alisema.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, alisema UWT imejipanga kuhakikisha CCM inashinda uchaguzi Mkuu kama ilivyoshinda kwa kishindo uchaguzi wa Serikali za mitaa ambayo wanawake wengine walijitokeza kugombea na kushinda.

Alimtaka Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kuzungumza kwa lugha ya staha na heshima kwa Rais Samia na kwamba upotoshaji unaofifisha kazi zilizofanywa na Rais Samia, UWT itazipinga kwa nguvu zote.

***Kwa maoni; +255 677 020 701 . Email; costumerrelations@guardian.co.tz***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Majaji wazingatie kauli ya Rais katika utendaji wa kazi

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria Nchini kwa mwaka 2025, yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma. Maadhimisho ya wiki hiyo ambayo hufanyika kila mwaka ni ishara ya kuanza kwa mwaka mpya wa Mahakama katika utendaji na utekelezaji wa majukumu yake.

Katika hotuba yake, Rais alizungumza mengi lakini kubwa ni kuwaonya majaji na mahakimu kuacha kuwa miungu watu katika utoaji wa hukumu bali watende haki kwa misingi ya sheria na Katiba ya nchi. Katika kufanya hivyo, aliwataka wanapoanza mwaka mpya wa mhimili huo, wazikague nafsi zao na kuweka dhamira ya kukaa daima kwenye upande wa haki.

Rais Samia aliwakumbusha majaji na mahakimu hao aliyozungumza Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mwaka 1984 katika Mkutano wa Majaji na Mahakimu kwamba wana dhamana ambayo inataka uadilifu na nidhamu ambayo haipaswi kutiliwa shaka. Samia aliungana na kauli hiyo akiwakumbusha kwamba kazi ya kutoa haki ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye mbali na utoaji haki, ana jaala na kudra ambavyo pia huvitumia kumkadiria mwanadamu.

Kwa mantiki hiyo, alisema majaji na mahakimu ni mawakala wa utoaji haki duniani lakini wamenyimwa jaala na kudra, hivyo wanapaswa kufanya kazi zao kwa kufuata makubaliano ya Katiba na sheria za nchi kama zilivyowekwa. Ili kutekeleza hayo, Rais aliwasihi majaji na mahakimu kuacha kuwa miungu watu katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Wakati mwaka mpya wa mahakama unaanza, kauli aliyoitoa Rais Samia imekuja kwa wakati mwafaka kwa sababu inawakumbusha magwiji na wabobezi hao wa taaluma ya sheria, walipewa kazi ya kuzitafsiri sheria kutambua yawapasayo kutenda. Wamepewa dhamana hiyo ili kutoa haki badala ya kupindisha sheria kwa maslahi yao na maswahiba zao.

Kwa muda mrefu, mahakama ni moja ya taasisi zinazolalamikiwa kuwa vinara katika rushwa na upindishaji haki kwa raia. Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Jaji Joseph Warioba, mwaka 1996 wakati wa warsha ya wanahabari katika mapambano dhidi ya rushwa, aliwahi kusema wananchi wamekata tamaa dhidi ya mahakama.

Jaji Warioba alibainisha kuwa watu wanaamini kuwa mahakamani kuna sheria lakini hakuna haki. Hali hiyo imesadifu kwa muda mrefu kutokana na uhalisia kwamba baadhi ya majaji na mahakimu wamekuwa wakidaiwa kupindisha sheria kwa maslahi binafsi. Pia baadhi wamedaiwa kuwa wamekuwa wakiandaa hukumu mbili- zinazohusu pande husika na mwenye fedha nyingi ndiye anayepewa ushindi.


Kutokana na kuwapo kwa dhana hizo na hata baadhi ya majaji na mahakimu kuonekana kwamba ni miungu watu, ni wakati mwafaka wa kubadilika na kufanya kazi kwa weledi hasa majaji warejee viapo vyao walivyovitoa wakati wa kuapishwa kuanza wajibu huo.

Kuna msemo katika Biblia Takatifu kuwa "Haki huinua taifa bali dhambi ni aibu kwa wote.' Msemo huo unabainisha kuwa iwapo taifa litakuwa na watenda haki wasioshawishiwa kwa rushwa, hakika haki itapatikana na kutakuwa na sifa kwa taifa hilo. Lakini pale haki inapopindishwa na kukawapo kupindishwa haki kwa wanaostahili kuikosa na kuwanufaisha wasiostahili, ni dhahiri kutakuwa na aibu kwa mahakama yenyewe, jamii na taifa kwa ujumla.

Mahakimu na majaji, ni vyema wakazingatia viapo vyao ili kulinda heshima waliyo nayo katika jamii badala ya kuwapo baadhi ya watu wanaodhani kuwa kuwapo katika nafasi hizo ni kupata manufaa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka 48 CCM ijitafakari zaidi

**LEO** ni kilele cha maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa CCM baada ya kuunganisha TANU na Afro Shiraz Party (ASP), ya Zanzibar ambayo hadi leo imeendelea kuwa madarakani.

Umri wa miaka 48 ya CCM si haba, kwani kama ni mtu aliyezaliwa mwaka 1977, kwa sasa ni mtu mzima mwenye watoto na huenda pia amejukuu.

Chama hicho ni miongoni mwa vyama vichache vilivyopigania ukombozi wa barani Afrika ambavyo bado vinaendelea kuwa madarakani huku vingine vikiwa vimeshajifia.

Mbali na chama hicho, vyama vingine vya ukombozi ambavyo bado viko madarakani ni SWAPO ya Namibia, MPLA Angola, FRELIMO Msumbiji, ANC ya Afrika Kusini na ZANU PF cha Zimbabwe.

Wakati huu ambao CCM inasherehekea miaka 48 tangu kuzaliwa, ni vyema pia ikatumia nafasi hiyo kutafakari kilikotoka na kilipo sasa, kwani vyama vingi vikongwe kama chenyewe havipo madarakani.

Zipo sababu nyingi ambazo zimechangia baadhi ya vyama vikongwe kuondolewa madarakani kwa njia ya uchaguzi, ikiwamo kujisahau na kupoteza ushawishi mbele ya wananchi.

> **Zipo sababu nyingi ambazo zimechangia baadhi ya vyama vikongwe kuondolewa madarakani kwa njia ya uchaguzi, ikiwamo kujisahau na kupoteza ushawishi mbele ya wananchi.**

Vilevile, kuna vyama vingine ambavyo vimesambaratika kutokana na ujio wa kizazi kipya ambacho hakifuatilii historia ya ukombozi wa nchi zao na kutaka mabadiliko bila kujua faida na athari zake.

Kwa sababu hizo na nyingine nyingi, CCM haina budi kuangalia ni wapi ambako hakuko sawa na kurekebisha ili kuepuka kukumbwa na wimbi la kusambaratika kama ambavyo vyama vingine vya ukombozi vimepotea.

Mfano mmojawapo wa vyama hivyo ni pamoja na KANU ya Kenya, UNIP ya Zambia, MCP Malawi, BDP Botswana, UPC Uganda, CPP ya Ghana, SSP ya Somalia na PDCI kutoka Ivory Coast.

Lakini pia vyama vya FRELIMO cha Msumbiji, ANC cha Afrika Kusini na ZANU PF cha Zimbabwe ingawa bado vipo madarakani, vimekuwa vikikumbana na wakati mgumu katika uchaguzi.

Hiyo ni dalili mojawapo kwamba kuna wimbi la kuviondoa madrakani karibu vyama vyote vya ukombozi, ndio maana nikaeleza kuwa wakati huu wa maadhimisho ya miaka 48, CCM haina budi kuangalia ni wapi pa kurekebisha ili kiendelee kuaminiwa na Watanzania.

Baadhi ya viongozi wa CCM wamekuwa wakieleza sababu mbalimbali zinazokifanya chama hicho kuendelea kuwa madarakani kuwa ni kutoa fursa kwa wote bila kujali jinsi, watu kuwa huru kuchagua na kuchaguliwa.

Hapa mkazo wao ni kwamba kuna demokrasia kubwa iliyojengeka ndani ya chama hicho na kwamba CCM haina uongozi wa kifalme, bali wa kupokezana vijiti, huku kila kiongozi ambaye muda wake huisha, huwa anawapisha wengine wachukue nafasi.

Yote hayo yanaweza kuwa na ukweli lakini kwa kawaida jamii inapochoka huwa haiangalii imefanyiwa mazuri kiasi gani na ndio maana karibu vyama vyote vya ukombozi vimeondolewa madarakani.

Sababu zinaweza kuwa ni za wananchi kupenda mageuzi au mabadiliko ama kujaribu upande mwingine wa Shilingi katika madaraka, hivyo ili kusiwe na sababu hizo, ni kuendelea kuwaletea maendeleo.

Mabadiliko ya kisiasa hayaepukiki, lakini vyama tawala vikitekeleza kile ambacho wananchi wanahitaji, hasa umoja, mshikamano, amanani na maendeleo, vinajiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kuongoza.

HABARI KITAIFA

# Wauza mitungi ya gesi chuma chakavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Nishati na Madini imesema baadhi ya watu waliopewa mitungi ya gesi ya ruzuku wameshindwa kuijaza gesi na wengine kuiuza kama chuma chakavu.

Akiwasilisha bungeni juzi taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati hiyo kuanzia Februari 2024 hadi Januari 2025, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. David Mathayo, alisema hali hiyo inaisababishia serikali hasara na kuathiri juhudi za kufikia asilimia 80 ya mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

"Serikali ifanye tathmini ya matumizi ya mitungi iliyotolewa kwa bei ya ruzuku ili kubaini endapo malengo ya kutolewa kwake yanatekelezwa,"alisema.

Aliitaka serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wanaouza na kununua mitungi ya gesi ya kupikia kama chuma chakavu au matumizi mengine yasiyofaa.

Kuhusu matumizi ya gesi asilia kwenye magari, alisema mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia na hivyo kulazimika kuwekewa mfumo huo nchini kwa wastani wa sh.milioni mbili kwa gari dogo.

"Serikali ihamasishe uingizaji nchini wa vyombo vya moto vyenye mfumo wa kutumia gesi moja kwa moja na serikali iongeze mtandao wa bomba la kusafirishia gesi asilia katika mikoa mingine kutokana na kuwa na manufaa makubwa ikilinganishwa na kutumia magari kusafirisha gesi hiyo,"alisema.

Kuhusu utolewaji wa fedha za CSR katika miradi ya umeme na gesi asilia, alisema sheria ya Petroli ya mwaka 2015 inaweka masharti yanayomtaka mmiliki wa leseni pamoja na mwekezaji katika kitalu cha gesi asilia kuandaa mpango madhubuti wa uwajibikaji kwa jamii kwa kushirikiana na serikali za mitaa na vijiji husika ili kuwezesha kutolewa kwa CSR kulingana na mpango huo.

Alitaka serikali ifuatilie na kufanya uhakiki wa fedha za CSR zilizotolewa na kampuni zilizowekeza kwenye miradi ya gesi asilia mkoani Lindi na Mtwara kwa mwaka 2014 hadi 2022 ili kutathmini endapo kiasi kilichotolewa kilikuwa stahiki.

Katika hatua nyingine, kamati hiyo ilisema kampuni kubwa za uzalishaji wa dhahabu zimeshindwa kutekeleza kifungu hicho kwa madai ya kuzuiwa na mikataba na kampuni za nje ya nchi, zisiuze au kusafisha dhahabu inayozalishwa kwa kampuni au viwanda visivyo na ithibati ya London Bullion Market Association (LBMA), jambo linaloathiri kiwango cha dhahabu kinachonunuliwa na BoT.

Alisema serikali ihakikishe majadiliano baina ya BoT na kampuni hizo yanakamilika mapema ili kampuni hizo zianze kutekeleza masharti ya kifungu cha 59 cha sheria ya madini na hivyo kuwezesha upatikanaji wa dhahabu ya kutosha kwa BoT.



Mafundi wakikarabati kwa kuweka viraka kwenye barabara ya lami iliyoharibika, eneo la Jangwani Mafuso, Kata ya Jangwani, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wafanyabiashara waanza kurejea Soko la Kariakoo

**Na Joyce Lameck**

BODI ya Wakurungezi wa Shirika la Soko la Kariakoo, imeanza kurejesha wafanyabiashara kwenye soko hilo baada ya ukarabati kukamilika.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi, Hawa Ghasia, alisema wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. bilioni 28.03 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa soko hilo.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha hizo ambazo zilitumika ili kufanikisha mradi huu wa kimkakati wenye nia ya kulifanya soko la Kariakoo kuwa la kimataifa," alisema Ghasia.

Pia mwenyekiti huyo aliwataka wafanyabiashara wote wenye madeni kulipa kabla ya kurejea sokoni. Takwimu zinaonesha kuwa wafanyabiashara 366 wanadaiwa na shirika Sh. 358,571,106.85.

"Hii ni kutokana na mkutano wa bodi ya wakurugenzi ya shirika kukutana Januari 27, mwaka huu, ambapo pamoja na mambo mengine ilijadili na kuazimia kazi ya kuwarejesha wafanyabiashara kwenye Soko la Kariakoo ianze mapema Februari. Uamuzi huo unatokana na kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa soko sambamba na kukamilika kwa kazi ya uhakiki wa waliokuwa wafanyabiashara," alisema.

Ghasia alisema menejimenti inaratibu utangazaji wa majina ya waliokuwa wafanyabiashara kwenye soko hilo ambao wamekidhi vigezo na sifa za kurejeshwa baada ya uhakiki. Alisema uhakiki uliofanywa umebaini wafanyabiashara 1,520, wanatarajiwa kurejeshwa sokoni.

Pia alisema majina na fomu ya kujiunga vitatangazwa kwa umma kupitia vyombo vya habari ikiwamo tovuti ya Shirika la Masoko ya Kariakoo na tovuti ya OR- TAMISEMI.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara na wananchi kuwa Shirika la Masoko Kariakoo kwa kushirikiana na mamlaka zingine za serikali, ikiwamo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, itaendelea kutoa taarifa juu ya utaratibu utakaotumika kipindi chote cha kuelekea ufunguzi wa soko hilo.

Pia wafanyabiashara na wananchi wote wenye sifa za kuingia sokoni watatangaziwa utaratibu utakaotumika, hivyo shirika linawataka kuendelea kuwa na subira wakati mamlaka zikikamilisha taratibu.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Wabunge waibana PSSSF kutoza michango wastaafu

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

BUNGE limeazimia mambo matatu ikiwamo kuagiza Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kurejesha fedha za michango zilizolipwa na wastaafu badala ya waajiri.

Hatua hiyo imetokana na kubainika baadhi ya wastaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao, ili kulipwa mafao yao kinyume cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Sura 371.

Akiwasilisha jana bungeni taarifa ya mwaka ya Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alisema PSSSF inapaswa kurejesha na kuzidai fedha hizo kwa waajiri kama sheria inavyoelekeza.

"Kitendo hiki kinaondoa imani ya mwajiriwa kwa mfuko huo, hakipaswi kuvumiliwa na Bunge ambalo ndio lenye mamlaka ya utungaji wa sheria, kinakinzana na lengo la kuanzishwa kwa mfuko huo wa kuhakikisha ustawi wa wanachama," alisema.

Alitaja azimio jingine ni mifuko iache mara moja utaratibu wa kutoa Namba za Malipo kwa Wastaafu ili walipe michango ambayo haijawasilishwa na mwajiri wakati wakifuatilia mafao yao.

Pia alisema mifuko ichukue hatua kali za kisheria kwa waajiri wasiowasilisha michango kwa mujibu wa sheria.

Awali, mwenyekiti huyo alisema Juni, 2024 Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alielekezakamati hiyo kushugulikia suala la wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao, ili kulipwa mafao yao na ilitokana na Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko.

Kufuatia maelekezo hayo, alisema kamati ilialika wadau ikiwamo Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), pamoja na Umoja wa Wastaafu Tanzania (REAT) ambao walithibitisha wamepokea malalamiko ya wastaafu kutakiwa kulipa michango hiyo.

"Tumepokea ushahidi wa nyaraka za uthibitisho na upande wa serikali, ulieleza kuwa Sheria na Miongozo ya Mifuko hairuhusu mwanachama kulipa michango ya mwajiri ili alipwe mafao. Hata hivyo iliongezwa kuwa mazingira yanaweza kutokea na kusababisha wastaafu kulipa michango hiyo endapo wastaafu watatumia namba za malipo zilizotolewa na mfuko kwenda kwa mwajiri," alisema.

Alisema serikali ilieleza kuwa mfuko hutoa namba hiyo kwa mwajiri na mwajiri ndiye ambaye humpatia mstaafu namba hiyo ili alipe.

"Wastaafu hawa wanalazimika kulipa kwa kuwa hawana kingine wanachotegemea zaidi ya mafao yao. Suala hili si sawa hata kidogo hasa ikizingatiwa kuwa sheria haizuii mstaafu kulipwa mafao yake hata kama mwajiri hajakamilisha michango yake," alisema.

Alisema PSSSF inawawajibisha wastaafu kwa makosa yake ya kushindwa kusimamia sheria kwa kuhakikisha mwajiri anawasilisha michango yake kwa wakati.

"Aidha, kupitia nyaraka na mahojiano yaliyofanywa na wadau, kamati ilibaini kuwa suala hili limekuwa likifanywa na PSSSF, na hakuna ushahidi na vielelezo uliopata dhidi ya NSSF," alisema.

Alisema kitendo cha PSSSF kutengeneza mazingira ya kuwafanya baadhi ya wastaafu kulipa michango ya mwajiri ili kulipwa mafao yao.

## Mfumo taarifa kijiografia kuchangia uchumi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

SERIKALI imesema Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Kijiografia (NSDI) ni kiungo muhimu cha dira ya kimkakati ya uchumi wa kidigitali wa Tanzania 2024-2034 na kuchangia uchumi imara wa taifa.

Uanzishwaji Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Kijiografia ni jambo la kimkakati kwa maendeleo ya taifa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lucy Kabyemera, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa warsha ya wataalamu ya kuandaa NSDI jijini hapa.

"Kwa kifupi NSDI ni msingi wa kufanikisha malengo ya maendeleo ya Tanzania ikiwa ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 inayoandaliwa hivi sasa," alisema.

Kwa mujibu wa Kabyemera, mfumo wa NSDI utaiwezesha nchi kujua kwa mapana ufanisi na mipango ya maendeleo, rasilimali zote za nchi na athari za mabadiliko ya tabianchi, vikwazo vya uchumi na maendeleo ya nchi na kuboresha upatikanaji taarifa muhimu za kuimarisha mifumo ya usalama na uchumi wa nchi.

Aidha, Kabyemera alisema Sera ya Kitaifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) 2023 inasisitiza umuhimu wa kutumia teknolojia kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi hivyo mfumo huo unalingana kikamilifu na sera hii kwa kutoa miundombinu ya data ya kijiografia inayohitajika Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ikiwa ni kiwezeshi muhimu katika kupanga na kuanzisha NSDI.

Akigusia Dira ya Kidigitali ya Rais Samia Suluhu Hassan ya mwaka 2030, Kabyemera alisema inalenga kuiweka Tanzania kuwa kinara wa mawasiliano ya kidigitali na NSDI ni kipengele muhimu cha dira hiyo kwa kuwa itawezeshwa kuunganishwa taarifa za kijiografia katika huduma mbalimbali za kidigitali.

"Mfumo huo utakapoanzishwa utawezesha na kuhakikisha matumizi bora ya taarifa za kijiografia kwa ajili ya kufanya uamuzi wa kupanga mipango mbalimbali katika sekta zote za maendeleo ya uchumi wa nchi.



Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu akichangia taarifa ya kamati ya Bunge ya Afya na UKIMWI na ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, zilizowasilishwa Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kampuni 45 za Italia kuangalia fursa Dar

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI 45 kutoka Italia zinatarajiwa kuja nchini kushiriki katika kongamano la nne la biashara na uwekezaji litakalofanyika wiki ijayo jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo pia linatarajiwa kuvutia kampuni za Tanzania, wafanyabiashara na wawekezaji wa sekta mbalimbali, mitandao ya biashara ya kikanda na vyama vya ushirika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mnali, alisema kongamano hilo litaangazia fursa za uwekezaji ambazo hazijatambulika.

Alisema washiriki wa kongamano hilo wataangalia fursa ambazo hazijatumika kikamilifu nchini katika sekta mbalimbali zikiwamo teknolojia za kilimo na uchumi wa buluu ikihusisha utaalamu kwenye masuala ya mbolea, mifumo ya umwagiliaji, ufugaji, matumizi ya ngozi, ufugaji wa samaki na usambazaji.

Pia alisema uhusiano wa kiuchumi kati ya Italia na Tanzania umeendelea kukua kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni ambapo mataifa hayo yamekuwa yakifanya biashara ya fedha nyingi.

"Biashara baina ya nchi hizi mbili zimeimarika kwa kiasi kikubwa katika sekta mbalimbali, zikiwamo viwanda, kilimo, utalii, ushirikiano wa kiufundi, mashine, kemikali, vifaa vya umeme, dawa na bidhaa za chakula," alisema.

Alisema kuwa Tanzania inasafirisha bidhaa za kilimo, madini na maliasili kama vile kahawa, chai, pamba, samaki na vitu vya tahamani kwenda Italia.



# Walia hujuma, kupanda bei petroli, dizeli

**Na Cynthia Mwilolezi,**

NGORONGORO

SHUGHULI za usafirishaji wa abiria na matumizi ya vyombo vya moto katika Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, zinasuasua kutokana na uhaba wa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Uhaba huo wa huduma ya nishati unadaiwa kusababishwa na hujuma zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara ya mafuta hayo.

Kutokana na hali hiyo, nishati hiyo kwa sasa inauzwa kwa bei ya ulanguzi kati ya Sh. 4,000 hadi 5,000 kwa lita kinyume cha bei elekezi inayotolewa kila mwezi na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA).

Kwa mujibu wa bei elekezi ya EWURA ya Januari mwaka huu, petroli katika tarafa hiyo inapaswa kuuzwa kwa Sh. 2,941 kwa lita wakati dizeli ni. Sh 2,797, huku mafuta ya taa yakielekezwa kuuzwa kwa Sh. 2,851 kwa lita moja.

Tarafa ya Loliondo, ndiko yalipo makao makuu ya Wilaya ya Ngorongoro na ina vituo viwili vya kutoa huduma ya mafuta kwa shughuli za serikali na watu binafsi.

Inaelezwa kwamba magari ya serikali yameendelea kupata huduma hiyo katika vituo hivyo, lakini watu binafsi wakiwamo waendesha bodaboda, hulazimika kununua kwa bei ya magendo mitaani kwa kati ya Sh. 4,000 hadi Sh. 5,000.

Mmoja wa waendesha bodaboda katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Wasso, aliyejitambulisha kwa jina moja la Msenii, alisema kuwa wananunua mafuta kwa bei ya ulanguzi kutoka katika makazi ya watu.

"Ukienda kituo cha mafuta unaambiwa hakuna mafuta hivyo tunalazimika kununua vichochoroni kwa Sh.4000 hadi Sh. 5000 kwa lita na wakati mwingine kama wana wasiwasi nawe wanakunyima.

"Juzi kulikuwa na mafuta kidogo katika moja ya vituo na tulikaa hapo katika msururu wa kusubiri kwa saa zaidi ya tatu na baadaye tukaambiwa yameisha. Hii ni kero kwetu na wateja wetu kwani tunalazimika kupandisha bei ya usafirishaji ili tupate marejesho na hela kidogo ya kulisha familia," alisema.

Hivyo, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati suala hilo kwani hali imekuwa mbaya.

Alipoulizwa kuhusu uhaba huo, Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Lovirii Long'idu alisema atafuatilia malalamiko hayo ya wananchi ingawa hawana taarifa za uhaba wa mafuta wilayani humo.

"Sisi tuna utaratibu na mifumo ya kujua kiasi cha mafuta kilichopo kila mahali na hata sasa Loliondo yapo mafuta ya kutosha lakini ngoja tufuatilie," alisema.

Alipoulizwa kuhusiana na kadhia hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo, alisema kwa rekodi zilizopo mafuta yapo ya kutosha wilayani humo na siyo kama inavyoelezwa.

"Ni kweli kuna changamoto zinazosababisha upungufu wilayani kwetu lakini hazijafikia hatua ya mafuta kuuzwa kwa ulanguzi vichochoroni. Ni kosa la kuuza mafuta bila kibali na leseni na katika vituo ambavyo havikuruhusiwa hivyo nimeagiza vyombo vinavyohusika kufuatilia na kuchukua hatua zinazostahili," alisema.

Mmoja wa wasaidizi wa mmiliki wa kituo kimoja cha mafuta katika tarafa hiyo ambaye hakutaka jina lake litajwe alisema kuwa uhaba huo unasababishwa na gharama kubwa wanazotumia kusafirisha mafuta kutoka Bandari ya Tanga hadi Loliondo.

## W'biashara wakoshwa urejeshaji mnada wa tanzanite

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAFANYABIASHARA wa madini ya tanzanite katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani mkoani Manyara, wamesema wameridhishwa na mnada wa madini uliorejeshwa na serikali, baada ya wazawa kuuza vito vya Sh. milioni 21.4.

Mnada huo uliondaliwa na kampuni ya Chusa Mining Ltd, umewezesha kuuzwa tanzanite yenye uzito wa gramu 4,874.16 na kuongeza mapato ya serikali kufikia Sh.milioni 1.5

Wakizungumza baada ya kufanyika kwa mnada huo, baadhi ya wafanyabiashara hao wamempongeza mkurugenzi wa kampuni hiyo kwa kutoa madini yake kwenye mnada huo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Sila Akede, alisema kitendo cha Chusa Mining Ltd, kutoa madini yake ili yauzwe kwa kufanyiwa mnada kwa wafanyabiashara hao kinapaswa kupongezwa.

Alisema umefika wakati kwa wachimbaji madini wengine, ambao migodi yao inazalisha kuwaunga mkono wafanyabiashara wa tanzanite kufanya minada kila wakati.

Mfanyabiashara mwingine, Ambrose Ndege, alimpongeza mchimbaji wa madini Mwakipesile, kupitia kampuni yake kwa kufanikisha mnada huo.

Naye Lidya Mollel, alisema minada kama hiyo inapaswa kufanyika kila mara ili kuchochea uchumi wa eneo hilo.

Alisema endapo minada hiyo itaendelea kufanyika itasaidia kukuza uchumi pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi wa eneo hilo.



Diwani wa Kata ya Mtindiro, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Mustapha Hatibu (kulia), akizungumza na viongozi wenzake, walipotembelea kukagua madarasa mabovu matano ya Shule ya Msingi ya Mgoda, kijiji cha Mtindiro juzi na kusababisha wanafunzi 360 kusomea katika madarasa mawili kwa zamu, asubuhi na mchana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Usanifu, upanuzi mradi wa maji miji 28 waanza

**Na Mwandishi Wetu,** KILINDI

AGIZO la Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kufanya usanifu wa upanuzi kwenye mradi wa maji wa miji 28 kutoka Handeni kwenda wilayani Kilindi limeanza kutekelezwa.

Kwenye taarifa ya RUWASA iliyowasilishwa jana na Kaimu Meneja wa Wilaya ya Kilindi, Philipo Bajuta katika Baraza la Madiwani alisema, Ofisi ya Meneja wa RUWASA Kilindi kwa kushirikiana na Ofisi ya Meneja RUWASA, Mkoa na HTM, wameanza kutekeleza agizo la Waziri wa Maji.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Waziri wa Maji, alitoa agizo hilo katika ziara yake ya Novemba 17, 2024 akitaka kufanyika usanifu wa upanuzi wa mradi wa maji wa miji 28 kutoka Wilaya ya Handeni kwenda Kilindi.

Imeelezwa kuwa usanifu wa ujenzi wa mradi huo utaziunufaisha kata nane za Wilaya ya Kilindi ambazo ni Jaila, Saunyi, Mkindi, Mabalanga, Msanja, Kwediboma, Kisangasa na ile ya Kibirashi ni ili kufikia lengo la serikali kuhakikisha huduma ya maji inafikia asilimia 85 ifikapo Desemba 2025.

Aidha, mapendekezo ya mpango wa utekelezaji bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) utatumia Sh. bilioni 4.7.

Katika fedha hizo kutoka serikali kuu na mfuko wa maji ni Sh.bilioni 2.2 fedha za wafadhili Sh. bilioni 2.4, Sh. bilioni 4.1 ni kwa ajili ya miundombinu na Sh.milioni 617 kwa uendelezaji miradi ya utafiti, usanifu na uendeshaji ofisi.

Kuhusu miradi ya maji inayoendelea katika Wilaya ya Kilindi itakamilisha ujenzi kupitia fedha za mfuko wa maji yenye thamani ya Sh.bilioni 33.8 na miradi hiyo ni Kwamaligwa na Diburuma/ Songe.

Mingine ni mradi wa maji ujenzi wa Bwawa la Saunyi (Lombout) na pia uchimbaji wa visima 19 katika vijiji 19, huku wilaya hiyo ikitarajiwa kuendelea kufanya utekelezaji miradi mipya.

Kwa upande wa miradi mipya ya maji, Wilaya ya Kilindi itaitekeleza kupitia Fedha za Mfuko wa Maji (NWF) na Serikali Kuu (GoT) yenye thamani ya Sh.bilioni 11.6.

Kaimu Meneja wa RUWASA wilayani Kilindi, Philipp Bajuta, alimhakikishia mjumbe huyo wa Kwediboma kuwa tayari mtambo wa kuchimba kisima unaendelea kwenye mji huo wa Kwediboma, huku ukiwa unaendelea kufanya kazi hadi maji yatakapopatikana.



# Familia yaiomba serikali kuingilia mgogoro na mwekezaji wa madini

**Na Remmy Moka**

FAMILIA ya mzee Raphael Gombanila kutoka Kijiji cha Mnekezi mkoani Geita wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro baina yao na mwekezaji anayedaiwa kuendesha shughuli za uchimbaji madini katika makazi yao, bila kufuata taratibu za kisheria.

Akizungumza juzi nyumbani kwake, mjane Mwamvula Kachila alisema wamekuwa wakiishi katika eneo hilo kwa muda mrefu ambako kuna makaburi ya baba yao mzazi aliyefariki mwaka 1984 pamoja na ndugu wengine.

Alisema baada ya kubainika kuwa eneo hilo lina madini ya dhahabu limechukuliwa na mtu ambaye anatajwa kuwa mwekezaji na wao kuzuiliwa kulitumia.

"Eneo hili liligundulika kuwa na madini ya dhahabu mwaka 2022 wakati tukichimba choo baada ya hapo alikuja akiwa na nyaraka kuwa anamiliki leseni halali ya uchimbaji katika eneo letu bila ridhaa wala matakwa yetu," alisema Mwamvula.

Mtoto wa mzee huyo, Mayala Kombanila alisema awali alipogundua kuwapo kwa madini hayo alitoa taarifa serikalini na waliendelea na uchimbaji katika eneo hilo kwa muda mrefu, lakini baadaye walitolewa na mwekezaji huyo ambaye baada ya kufuatilia waliambiwa kuwa mtu huyo ana leseni halali ya hilo eneo.

"Tumekuwa tukitishwa kwa muda mrefu kutoka katika eneo hilo tukitakiwa kutoka kwa kuliacha eneo. Tunaomba serikali kuingilia mgogoro huu ili taratibu za kisheria zifutwe," alisema Mayala.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mikezi, Felicia Mlazi alikiri kupata taarifa hizo kabla hajawa Mwenyekiti wa Kijiji hicho na hadi sasa taarifa ameendelea kuisikia, huku akieleza kuwa kuna baadhi ya familia zilizolipwa kwa ajili ya kuondoka katika eneo hilo.

"Kuna wakazi walilipwa fidia ili kuondoka katika eneo hilo la uchimbaji lakini kama kuna familia ambayo haijalipwa na inamalalamiko ni vyema kafika ofisini kwani hadi sasa hakuna familia ambayo imefika ofisini kwangu lakini nimekuwa nikisikia malalamiko hayo," alisema Mlazi.

Naye Diwani wa Kata Kaseme, Andrew Kalumula, alisema suala hilo limekuwapo kwa muda mrefu na kuiomba Wizara ya Madini kufika katika eneo hilo na kutoa elimu na kuwaelewesha wananchi juu ya umiliki wao wa ardhi yenye madini na taratibu zake.

Alisema wakati mwingine wananchi wamekuwa wakidhurumiwa na wadau wanaochukua maeneo hayo hasa katika tathmini ya thamani ya ardhi, kwamba imekuwa haitendi haki kwa wananchi kutokana na maeneo yenye rasilimali kutolipwa kwa usawa stahiki.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani humo jana, wakati akitoa taarifa ya utendaji kwa kipindi cha robo ya pili kuanzia Oktoba hadi Desemba 2024/2025, kwamba wamefanikiwa kuokoa Sh. milioni 137.8 ya mauzo ya viwanja katika Manispaa ya Kahama. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Utiririshaji majitaka wawakera wananchi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa mtaa wa Shunu Manispaa ya Kahama, wameiomba serikali kufuatilia na kudhibiti vitendo vya baadhi ya wananchi kutiririsha majitaka wakati wa mvua, hali inayohatarisha afya zao.

Waliwasilisha kero hiyo juzi kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipasha juu ya hali ya utunzaji wa mazingira katika kipindi hiki cha mvua ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko katika mtaa huo.

Mkazi wa mtaa huo, Radegunda Shayo alisema licha ya juhudi mbalimbali za kusafisha mazingira bado kuna baadhi yao wamekuwa na tabia ya kutiririsha majitaka kutoka vyooni hasa kipindi cha mvua na kuelekeza kwenye makazi ya watu.

Alisema hali hiyo inatishia kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko na kuwa wamekuwa wakitoa taarifa kwa viongozi wa serikali za mitaa, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi yao.

John Bulege alisema licha ya utiririshaji majitaka hayo bado pia kuna tatizo la kaya kukosa vyoo na kuiomba idara ya afya kukagua ujenzi wa makazi unaoendelea, kwani nyumba nyingi zimekamilika lakini hazina vyoo.

Mkazi mwingine Paschal Joseph alisema: "Mvua ikikata mitaro na mifereji hapa inaanza kutoa harufu mbaya tunaishauri idara ya afya kwa kushirikiana na wataalamu wa mazingira kudhibiti suala hili".

Ofisa Afya na Mazingira wa Manispaa ya Kahama, Basil Kafunja, alisema zaidi ya asilimia 85 ya kaya zina vyoo bora na wanaendelea kuwasisitiza wananchi kujenga vyoo bora ili kudhibiti magonjwa yanayotokana na uchafuzi wa mazingira.

Alisema kutiririsha maji machafu na maji taka yanayotoka vyooni ni kosa la jinai, suala la usafi wa mazingira ni mtambuka na kuzitaka kamati za afya ngazi za kata, mitaa na vijiji kuhakikisha wanadhibiti suala hilo.

# Halmashauri ya Bukoba yatoa mil. 520/- vikundi 79

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Bukoba, Jacob Nkwera, amesema halmashauri hiyo imetoa Sh. milioni 520 kwa vikundi 79 kati ya vikundi 300 vilivyoomba mikopo ya asilimia 10.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipasha kuhusu maboresho ya utolewaji wa mikopo hiyo kwa mwaka 2025, kueleza kuwa katika ya vikundi hivyo ni 224 pekee vilivyokidhi vigezo na kati ya hivyo 79 vilipewa mikopo.

Alisema utoaji wa fedha hizo ulizingatia idadi sawa ya utoaji mikopo na kuwa vikundi 79 vimepewa kwa awamu ya kwanza vikijumuisha wanawake 42, vijana 32 na wenye ulemavu sita.

Alisema wanawake walitengewa Sh.milioni 208, vijana Sh. milioni 208 huku wenye ulemavu wakipangiwa Sh.milioni 104 ambayo yote imetolewa kuanzia Januari, huku wakitakiwa kurejesha Februari.

Kuhusu usimamizi wa urejeshwaji wa fedha hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Siima, alisema fedha hiyo inayotolewa kwenye mapato ya ndani wamejipanga kusimamia vikundi vyote virejeshe katika muda sahihi.

"Kama umekopa mkopo urejeshe kwa wakati na kama umekopa hupendi kufanya chochote ni vizuri uchukue halafu uweke katika akaunti husika ili ujiepushie usumbufu wa baada ya fedha hiyo kuhitajika na ukawa umeshaitumia," alisema Siima.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo akiwamo Sylivanus Richard mkazi wa Kata Buhembe alitaja muda uliowekwa kwa ajili urejeshaji ni mzuri na utawasaidia kuwa na matumizi mazuri.

Alisema: "Lengo la utafutaji mtaji ni kuongeza pesa ambao tayari imeshatafuta hivyo fedha hizo tulizozipata ni kwa ajili ya kuongeza kwenye kile ambacho tumekianzisha na ndani ya muda uliowekwa tutakuwa tumepata matokeo ya fedha hiyo".




Ukurasa 14

**UBABE MAREKANI**

**YAJAYO YANASIKITISHA A/KUSINI**

**YABANWA CHINA, EU ZIKIKAANGWA**



Ukurasa 12

**Vita vya DRC Ukanda Maziwa Mkuu hatarini**

**siasa**

JUMATANO FEBRUARI 5, 2025

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

MIAKA 30 YA BEIJING

# ‘Liwike lisiwike uwezeshaji watoto wa kike haukwepeki’

**Na Mwandishi Wetu**

KUKOSOA juhudi za kuwawezesha watoto wa kike kwa madai kuwa zinalenga kufanya mapinduzi ya kufanikisha wanawake kutawala wanaume kunaanza kusikika.

Ni maoni yanayosikika miongoni mwa wanaopinga harakati za kuwainua wasichana na kuondoa mifumo kandamizi inayosababisha wawe mbumbumbu, maskini na kuendelea kuumizwa na ukatili wa kijinsia.

Hisia hizo zinatumiwa na watu wanaobanwa na lawama za kushindwa kuondoa unyanyasaji na misemo hiyo inadhihirisha kuna baadhi ya Watanzania hawataki kuona maisha ya mwanamke yakiboreshwa.

Mazoea ndani ya miongo mingi ya unyanyasaji wanawake na watoto inasababisha kuwaza kuwa kuwezesha wasichana ni mkakati wa kuwaandaa kuwakandamiza wanaume, wakati sivyo.

Balozi Getrude Mongella, Mwenyekiti wa Mkutano wa Beijing uliofanyika 1995 nchini China ambao leo umetimiza miaka 30, anachambua hoja hiyo.

Ajenda kuu ya mkutano huo ni kuona dunia isiyo na ubaguzi wa kijinsia, kadhalika uwezeshaji wanawake na mtoto wa kike kwa hali zote unafanikiwa, anafafanua.

Balozi Getrude anakiri kuwa Beijing imeleta mapinduzi makubwa ya kifikra kwa kuwezesha serikali kutambua kuwa wanawake na wanaume wana haki sawa kama raia wa dunia moja.

Aidha, kutambua kwamba, wanawake ni wakazi wa dunia hii kama wanaume na kwamba dhamira ya mkutano haikuwa kubadilisha mfumo kandamizi na kusimika utaratibu kandamizi mwingine ili wanawake wachukue nafasi ya kunyanyasa wanaume.

Anasema lengo la mkutano na utekelezaji wa maazimio ni kujenga usawa wa jinsia kwa wanawake na wanaume, watoto wa kike na wa kiume bila ubaguzi.



Ndoa za watoto ni suala lisilokubalika na maazimio ya Beijing. **PICHA: MTANDAO**

**MTOTO WA KIKE KWANZA**

Kumwezesha si kukurupuka ni moja ya masuala 12 yaliyobainishwa katika tamko la Beijing mwaka 1995, baada ya kubaini kuwa mifumo kandamizi inawaathiri watoto, lakini kwenye mfumo dume mtoto msichana anaatharika maradufu.

Mfano, anabaguliwa hana haki ya kurithi, kielimu mwanaume anapendelewa zaidi asome, anafanyiwa ukatili wa kimwili, hukeketwa, kubakwa, kuozwa utotoni na kunyimwa haki nyingi za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mathalani, Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2022, inaonyesha kuwa mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni, Songwe ikiwa kinara yenye asilimia 45.

Inamaanisha kila watoto wa kike 100, karibu nusu au 45 wamenyanyaswa na kupewa mimba utotoni.

Ruvuma ni ya pili kwa asilimia 37, Katavi 34, Mara 31 na Rukwa asilimia 30.

Hizo si habari njema baada ya miaka 30 ya Beijing inayosisitiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji mtoto wa kike na maendeleo endelevu kwa wote. Hivyo kuwezesha watoto wa kike si hiari ni lazima.

Profesa Ruth Meena kutoka Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, anafafanua maana ya kuwezesha mtoto msichana kuwa ni kumjengea uwezo wa kuuthamini mwili wake, kuulinda utu wake, kuutetea na kukataa kutumiwa kuumizwa iwe kimwili, kisaikolojia au kiuchumi.

Anafafanua kuwa binti aliyejengewa uwezo anathamini utu wa wote wakiwamo watoto wa kiume, hawanyanyasi, kukandamiza wala kuwadharau wengine, bali ni mtetezi wa haki zake na za binadamu.

Anasema uwezeshaji hauathiri wala kupokonya uwezo wa watoto wa kiume kwa sababu wamelelewa na kukuzwa kwenye mazingira na fikra za kuheshimu ndugu wa kike kuanzia mama zao hadi shangazi.

Baadhi ya wanafunzi wanaosoma katika kituo cha elimu cha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima cha Tumbi Sekondari, mkoani Pwani, wanaorudi darasani baada ya serikali kuwawezesha waendelee na masomo ni mashahidi.

Wanaamini kuwa kupata mimba si mwisho wa maisha kwa sababu wamepata nafasi ya pili na sasa wanatimiza ndoto zao bila kukatishwa tamaa, kwani mtoto wa kike ameona alipokosea, akipaepuka na sasa yuko tena shule.

“Baada ya kupata mimba nilirejea nyumbani nikawaomba msamaha wazazi, wamenilea na mwanangu nilipojifungua. Baada ya miaka miwili wamenitafutia shule ninaendelea na masomo.” Anasema, mwanafunzi wa taasisi hiyo ya elimu, kituo cha Tumbi Sekondari, jina tunalihifadhi.

Kuanza kwake masomo ni uwezeshaji wa watoto wa kike kupitia program ya‘re-entry’ inayolenga kuwarejesha shuleni wasichana wanaokatizwa masomo kwa sababu yoyote, mpango unaoanzishwa na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Mwanafunzi mwingine anaeleza kwamba baada ya kupata mimba alifukuzwa na baba yake akakimbilia kwa mjomba aliyemlea hadi kujifungua na sasa amemsajili kituo cha Tumbi Sekondari anasoma.

Mifumo kandamizi bado inajitokeza, licha ya serikali kuruhusu wasichana warudi shuleni baada ya changamoto kama mimba, kukosa ada au umbali wa shule inaendelea kuwazuia ni wakati wa kubadilika jamii

INAENDELEA UK. 12

# Vita vya DRC Ukanda Maziwa Mkuu hatarini

**Na Mwandishi Wetu**

NCHINI Congo DRC ni vilio, watu duniani wakiangalia runinga machozi yanawatoka wakisikitika ni miaka mingi zaidi ya 20 nchi hiyo imejaa ghasia na hata leo hali ni tete.

Waasi wa M23 wa Congo wanatishia amani ya ukanda mzima wa Afrika Mashariki na Maziwa Makuu na kuongeza hofu.

**ATHIRI KIKANDA**

Mataifa jirani yanaugulia kwa sababu mashambulizi yanasababisha mamilioni ya wakimbizi kutoka maeneo yote ya Kivu Kusini na Goma kutawanyika Afrika Mashariki.

Wakongo hao wanakikimbilia Rwanda, Uganda, Burundi, Tanzania na Kenya.

Katika kujiokoa kila kitu kinavuka mipaka kuanzia silaha ndogo na kubwa yote hayo yakitishia usalama. Uwezekano wa kuongezeka uhalifu na uporaji na hata mauaji kutumia silaha.

Vita vinavuruga uchumi eneo la Maziwa Mkuu. Jambo lisilopingika ni kushuka shughuli za kibiashara kutokana na kukosa usalama, kwenye makazi, vituo vya kuuza na kununua miundombinu ya usafirishaji.

Uharibifu wa mazingira hasa kukata miti na kuvamia mapori ili kupata makazi na shughuli za wakimbizi ni mambo yasiyokwepeka ukanda wa nchi jirani.

Vita vinavuruga usafiri wa watu pamoja na bidhaa hasa mipakani hata angani kwa vile upo uwezekano wa kushambuliwa.

Jamii wenyeji kukosa amani na utulivu kutokana na kufurika kwa watu wageni kwenye makazi au maeneo yao.

Mwaka 2025 umeanza vibaya DRC kutokana na ubabe wa waasi hao ambao wameua watu zaidi ya 700.



Waasi wa M23 wanaoendeleza vita DRC. **PICHA: MTANDAO**

Wanatamba kuwa watasonga mbele tena wakiapa kupigana hadi kutwaa mji mkuu wa Kinshasa.

Waasi wakidaiwa kuungwa mkono na Rwanda wanatangaza kuendeleza vita vyao hadi mji mkuu Kinshasa, ambako Rais Tshisekedi anatoa wito wa kuajiri wanajeshi wapya katika kukabili vita dhidi yao.

Mji wa Goma kuangukia tena mikononi mwa waasi wa M23 kunaongeze mawimbi ya mshtuko, hofu na wasiwasi katika eneo la Maziwa Makuu na hatari ya kuzusha vita vinavyoweza kuenea ukanda mzima.

Wacongo wanazidi kuteseka wakikumbuka vita vya mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2000 ambapo wanajeshi wa mataifa saba ya Afrika yaliingilia kati na kurejesha amani.



Vita hivyo vilisababisha Wakongo milioni 5.4 kuuawa.

Mapambano hayo yanayoendelea yanatisha hasa kwa sababu M23 imekuwa ikiendeleza uasi huo kwa miaka mingi ikidaiwa inaungwa mkono na Jeshi la Ulinzi la Rwanda (RDF), lengo likiwa kutetea maslahi ya Rwanda.

Kuna madai kuwa kati ya wanajeshi 6,000 wa M23, kuna takriban wanajeshi 4,000 wa Rwanda.

Aidha, upo ushahidi kutoka kwa uchunguzi wa Umoja wa Mataifa kwamba M23 inapokea msaada kutoka Uganda.

Ripoti zinaonyesha kuwa wanajeshi wa Kongo, wanamgambo wanaoungwa mkono na serikali wanaojulikana kwa jina la Wazalendo, na mamluki wa kigeni wamejisalimisha kwa wanajeshi wa RDF nchini DRC.

Mkakati na mpango kabambe wa kuiteka Goma, mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini wenye utajiri mkubwa wa madini mashariki mwa DRC, umefanikiwa na sasa waasi wanaendelea kukoleza mashambulizi waliyoyaanzisha tangu 2022 wakikamata na kudhibiti eneo la mashariki mwa Congo.

Hatua hiyo inahusishwa na juhudi za kuanzisha utawala mwingine wa eneo huru lisilofungamana na serikali ya Kinshasa, kwa sababu unayahusu maeneo yanayodhibitiwa na M23 wakilenga upanuzi wa miradi ya kuchimba madini.

Hii inamaanisha kwamba kundi la waasi na wanaowaunga mkono wana malengo ya muda mrefu katika kushikilia na kuongeza zaidi himaya yao na kufanikisha udhibiti wao wa kijeshi.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN) zaidi ya watu 500,000 wamekimbia makazi yao tangu kuanza mwaka huu, wakati maelfu wakifikishwa hospitali ambazo zimezidiwa na majeruhi, wengi wao wakiwa raia.

Biashara zinakwama maduka hadi kwenye uzalishaji kumefungwa kutokana na mapigano makali ambayo pia yanaua walinda amani 17 wakiwamo kutoka mataifa ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wanaoshiriki Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Utulivu DRC (MONUSCO).

Machi 2024, Umoja wa Mataifa uliripoti kwamba idadi ya wakimbizi wa ndani wa DRC ilifikia milioni 7.2 ukisema ni moja ya idadi kubwa zaidi duniani ambayo haijawahi kutokea.

UN inakadiria kuwa tangu 1996, vita mashariki mwa DRC vimesababisha takriban vifo milioni sita.

## 'LIWIKE LISIWIKE UWEZESHAJI WATOTO WA KIKE HAUKWEPEKI'

**INATOKA UK. 11**

iwaunge mkono watoto wa kike kuboresha maisha yao. Ikumbukwe wanasoma bila malipo serikali ikigharamia elimu yao.

Watetezi wa haki za mtoto wa kike wanasisitiza msichana akiwezeshwa haathiriki na mifumo au taratibu kandamizi mfano, kutoka mikoani kupelekwa mijini na kwenye majijini makubwa kuwa mfanyakazi wa ndani.

Akielimishwa na kuwezeshwa atapinga kubakwa na waajiri, watoto au ndugu zake wanaume, kupigwa, kunyimwa mshahara na kutumikishwa kama punda.

Anasema Farida Jackson, Ofisa Miradi wa asasi ya Initiative for Domestic Workers, inayotetea haki za watumishi wa ndani mkoani Pwani.

"Akielimishwa na kuwezeshwa atataka mazingira na kazi zenye staha na usalama, atadai mkataba wa ajira, atatoa taarifa akidhalilishwa na kutetea haki zake hata mahakamani."

"Zama lazima zibadilike siyo tena wakati wa kuwaacha watoto wa kike kutumiwa kingono nyumbani kwa watu mijini, wengine kwenye madanguro au ndani ya vibandaumiza mitaani na ajenda ni moja ya elimu na kuwawezesha ili sauti za wasichana na wanawake zisikike kwenye majukwaa makubwa kwa madogo kushangilia usawa wa kijinsia." Anasema Farida.

Wakiwezeshwa na kuelimishwa jamii haitaendelea kusikia habari za manusura wanawake na watoto wanaoishi na VVU na UKIMWI baada ya kupitia ukandamizaji na unyanyasaji kingono na kijinsia.

Kadhalika, mambo yatabadilika si kuwaona wakiishi kwa msaada wa mashirika ya kijamii na kupewa huduma za ushauri wa kisaikolojia, mafunzo na ujuzi wa maisha, badala yake watajitambua na kuepukana na madhila hayo. Huku wakiishi maisha bora kama raia bora wa dunia hii na Tanzania kama inavyoainisha Dira ya Maendeleo ya 2050, kuwa ni maisha bora kwa kila Mtanzania.

**LA MUHIMU**

Kuwa na bajeti za kijinsia, mfano ujenzi wa visima vya maji na vyoo vya wasichana vilivyo na vyumba maalumu vya kujisitiri wanapohitaji huduma hiyo, kama wanavyohimiza wanaharakati.

Uwezeshaji wa wanawake na watoto wa kike utaleta kujitambua na kunufaika na fursa za maendeleo zilizopo.

"AZAKI na serikali zikiwawezesha kujitambua watajua kuwa kazi yao si kutumiwa kuburudisha wengine.

Mfano kwenye sekta zinazokua kwa kasi za sanaa,burudani na utalii watabadilika kujua kuwa jukumu lao si kuuza vinywaji, au kuburudisha zaidi. Watatumia fursa kujiendeleza na kumiliki vitega uchumi." Anasema Najaha Bakari, Msemaji wa Baraza la Michezo la Taifa.

Anasema watakuwa watunga nyimbo si kuimba za wenzao, waandishi wa sinema akikumbusha kuwa uwezo mdogo kiuchumi, mapato duni na kukosa elimu vinachochea ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

Ni wakati wanaohofia juhudi za kuwezesha watoto wasichana washiriki kampeni za kuwashirikisha wazazi, walezi na jamii kubadilisha mtazamo huo na kuhimiza umuhimu wa elimu na maisha bora kwa watoto wote, bila ubaguzi wa kijinsia.

Elimu na uwezeshaji vinafanikisha kutambua na kuibua vipaji vya watoto wa kike, kuwajenga na kuwaendeleza kwenye eneo wanalolipenda na kulimudu ili walitumie kuendeleza maisha yao kwenye dunia ya sasa yeny furusa nyingi zinazotokana na vipaji.

**JUHUDI KITAIFA**

Tanzania imepiga hatua katika miaka 30 baada ya Azimio la Beijing kuwezesha watoto wa kike na kutokomeza ubaguzi wa jinsia, udhalilishaji na unyanyasaji watoto mfano, ipo sheria ya makosa ya kujamiiana ya 1998, inayoharamisha na kuadhibu ukatili kama ukeketaji na ubakaji.

Aidha, Zanzibar imeanzisha mahakama ya maalumu ya udhalilishaji Juni 2021 kusikiliza kesi za ukatili dhidi ya watoto.

Kuna sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inayobainisha na kulinda haki za mtoto. Kadhalika

Mahakama Kuu na ya Rufani zilibatilisha vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya 1971 inayoruhusu mtoto wa kike kuolewa chini ya miaka 14.

# CHADEMA inavyopigilia msumari 'no reforms no election'

Na Halfani Chusi

BAADA ya CHADEMA kumaliza uchaguzi na kusimika viongozi wapya, inageukia ajenda ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ikisema 'no reforms no election', kumaanisha bila mabadiliko hakuna uchaguzi.

Tundu Lissu Mwenyekiti Taifa CHADEMA, anasisitiza msimamo huo huku akisema muda uliopo unatosha kufanya mabadiliko wanayohitaji.

Lissu anasisitiza msimamo huo alipokabidhiwa rasmi uongozi wa chama hicho kwenye makao makuu Mikocheni jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Katika hotuba yake, anafafanua kwamba kuna uchaguzi mkuu Oktoba na kuna 'no reforms no election' hayo mambo mawili hayaendi pamoja na tafsiri yake kama hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi, si kwamba watasusia haki hiyo ya kidemokrasia.

"Sitaki nizungumze hapa zaidi tunaenda kujifungia tutaamua hautakuwa uamuzi wangu, bali wa chama, tutakaa na viongozi tutatoa msimamo," anasema akikaribishwa kwa kushangiliwa na wafuasi wa chama hicho waliofika kumkaribisha ofisini.

Anasema wanapaswa kuzungumza lugha pekee anayoweza kuielewa Rais Samia Suluhu Hassan na wataizungumza kwa nguvu kwa sababu hakuna yeyote anayetaka uchaguzi uwe kama wa mwaka 2020.

"Tutaonana na marafiki zetu duniani tuwaambie msimamo wetu hadharani tutawaomba watuunge mkono, na wale wasiotupenda tutawaangalia usoni kuwaambia msimamo wetu ni huu," anasema Lissu mwanasheria mbobezi.

Anatangaza kuwathibitishia wanaosema uongozi mpya ni wa wabangaziaji kwa kufanya kazi na kuleta mabadiliko ndani na nje ya chama.

Anapoulizwa kama msimamo huo utafanikiwa na kipi kipya kinachowapa ujasiri, anasema suala hilo linakwenda kutengenezewa mkakati na kamati kuu ilitoa azimio na mkutano mkuu umelikubali.

Anasisitiza msimamo huo wa 'no reforms na election' siyo wake bali ni wa chama na kwamba kazi yake ni kutekeleza maagizo ya CHADEMA.

Hata hivyo anasema hiyo haina maana hana mawazo yake juu ya msimamo huo, akitoa ufafanuzi zaidi.

Anaanza kuwahoji wafuasi wake "Mahali tulipo nani anaweza kasema tukienda kwenye uchaguzi ujao kwa sheria na tume iliyopo watapata chochote? Anyooshe mkono.

Wafuasi hao kwa sauti moja wanajibu "haiwezekani" hapo akasisitiza tukisema twende katika uchaguzi wao wanajua na Mungu anajua tunaenda kudhulumiwa na wengine kuumizwa.

Anasisitiza katika mazingira hayo, hawawezi kwenda kunyolewa tena na kwamba hawatokuwa kama kondoo anapelekwa kila siku machinjioni akiwa amenyamaza.



Tundu Lissu Mwenyekiti Taifa CHADEMA, aliyechaguliwa mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

> Anaongeza kuwa kutokana na hali hiyo, CHADEMA itawakumbusha wajibu wao na itawaondoa madarakani, akikumbushia kuwa Chalamila ni mteule wa Rais maana yake alichosema ni kauli yake.

"Ninaamini na nina ushahidi wa kutosha wa chaguzi tatu, wapo wanaounga mkono ninachokiamini 'no reform no election' tunazungumzia njia zisizo za kawaida za kufanya siasa, tunazungumzia kushurutisha mageuzi, kupata mageuzi kwa shuruti kama walivyopata Kenya, Malawi, bunge linaweza likakaa muda wowote hata bila kuwa na ratiba," anasema Lissu.

Katika kutetea hoja yake, anakumbusha kuwa bunge liliwahi kuitishwa kwa dharua Jumamosi ukumbini Karimjee kuidhinisha hoja ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar na hata leo upo.

"Katiba inasema bunge likivunjwa linaweza kuitishwa muda wowote kabla ya uchaguzi mkuu, na sisi tutanyamaza tukiwa tumekufa hata tukiwa gerezani tutapambana kutoka gerezani," anasema Lissu.

Anaeleza kuwa wakifanya harakati sawasawa anaamini mageuzi yatatokea na uchagzui utafanywa kukiwa na mfumo mpya.

Vilevile Lissu anawakaribisha watu wanotaka kujiunga na chama hicho akisema milango ipo wazi akisisitiza chama hicho kinahitaji jeshi kubwa na karama.

**WASIRA AGUSWA**

Makamu Mwenyekiti CHADEMA, John Heche, anatuma ujumbe kwa Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Stephen Wasira kwamba umri umesonga na hana jipya.

"Nimemuona mzee Wasira amekuwa serikalini kwa miaka 80 anataka atengeneze kama anashindana na mwenyekiti wetu Lissu, Wasira, Lissu si saizi yako, huyu anapambana na Rais Samia Suluhu Hassan si wewe.

"Hatuna nafasi ya Lissu kushughulika na wewe mmekuwa serikalini kwenye nchi iliyojaliwa rasilimali za kutosha lakini Watanzania wamebaki masikini kwasababu ya mawazo ni yaleyale yaliyoshindwa."

Anadai wanafanya mabadiliko kwa viongozi wale wale Wasira ni yuleyule, hawezi kuleta mabadiliko, ameshiba kwa sababu analipwa mshahara tangu akiwa na miaka 20 mapaka leo akiwa na miaka 80 na hajui vijana wanavyotaabika.

Anaongeza kuwa ni shibe hiyo, ndiyo maana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alimjibu ovyo mjamzito aliyepiga simu akilalamikia kukosa huduma za uzazi katika hospitali ya umma.

"Mgonjwa alimpigia simu kumwambia hana 'gloves' akamjibu amwambie mume wake achukue mkasi amzalishe hebu fikiria kiwango hicho cha uongozi kwa hali hiyo. Hawa ni watu waliojisahau kwa kiwango kikubwa," anasema Heche.

Anaongeza kuwa kutokana na hali hiyo, CHADEMA itawakumbusha wajibu wao na itawaondoa madarakani, akikumbushia kuwa Chalamila ni mteule wa Rais maana yake alichosema ni kauli yake.

Anatamba CHADEMA inarejea kufanya kazi yake, huku akilihadharisha Jeshi la Polisi kuwatisha kwa kuwa ni chama kilichosajiliwa kisheria.

Anasema hakuna mwanachama atakayepata upendeleo katika nafasi fulani kwa sababu alimuunga mkono Lissu au yeye na hivyo uwezo ndio utamweka katika nafasi ya uongozi.

Chama hicho, kimekuwa imara na kitaendelea kubaki imara huku akiwataka wafuasi wake kuondoa shaka kuwa kitakufa.

**KUANDAA MKAKATI**

Katibu Mkuu John Mnyika anasema CHADEMA na viongozi wapya na wastaafu watajifungia ndani kwa wiki moja kuandaa mkakati wa pamoja kuelekea uchaguzi mkuu.

"Uongozi huu ni wa awamu ya saba ni mpya lazima tupate wasaa kukaa kupanga mipango kesho tutajifungia viongozi wakuu wote wastaafu kwa pamoja tutatoka na mwelekeo mpya tutaanza kuzunguka kuendesha mapambano katika taifa letu."

Kuhusu mkutano wake kuzuiwa na Jeshi la Polisi siku chache zilizopita anasema, alitaka kueleza mambo ya kuyapatia kipaumbele na ujio wa mwenyekiti wa katika ofisi za chama.

Aidha, anatumia mkutano huo kulaani kitendo cha jeshi hilo kuzuia waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao kwa kuwa sheria inawaruhusu.

"Polisi waliweka 'difenda' karibu na geti la kuingilia wakaanza kuwazuia waandishi wa habari kufanya kazi yao wakati hata katikati ya vita wanaruhusiwa kutimiza majukumu yao.

Anasema watajifungia kuanzia viongozi wote na wastaafu kwa ajili ya kupanga mipango kwa pamoja kutoka na mwelekeo mpya, baada ya hapo wataanza kuzunguka kuendesha mapambano katika taifa.

Anawataka wana-CHADEMA kuachana na tofauti zilizojitokeza wakati wa uchaguzi na badala yake wasonge mbele kwa nguvu ya pamoja kufanikisha agenda ya mageuzi.

Kuhusu aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe kutoonekana wakati wa makabidhiano ya ofisi anasema katiba ya chama chao inaruhusu Katibu Mkuu kusimamia na kwamba hakuna shida kama watu wanavyodhani.

Chama hicho kimefanya uchaguzi kwa kumchagua Lissu kuwa Mwenyekiti Taifa ambaye awali alikuwa Makamu akichuana na aliyekuwa Mwenyekiti Mbowe.

Ni uchaguzi ambao wajumbe walikesha kusubiri hatima, Lissu akiibuka mshindi kwa tofauti ya kura 31.

UBABE MAREKANI

# Yajayo yanasikitisha A/Kusini yabanwa China, EU zikikaangwa

**Na Christina Mwakangale**



Marais Donald Trump wa Marekani (kulia) na Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini wapo kwenye msuguano wa kisera. **PICHA: MTANDAO**

DONALD Trump, ndiye Rais wa Marekani wa 47 ambaye tangu aingie ofisini wiki mbili sasa amekuwa gumzo duniani, akigusa nchi zinazoendelea na zilizoendelea.

Mashirika, watu binafsi, taasisi za umma na serikali za nchi zinazoendelea na zilizoendelea zimepata 'meseji' ya msimamo wa Marekani kutoka Ikulu ya White House, ambayo aliirejea tena Januari 20, mwaka huu.

Baada ya kuapishwa tu, alitia saini msururu wa hatua za kiutendaji, ikiwa ni pamoja na kutangaza hali ya dharura ya kitaifa katika mpaka wa Marekani na Mexico na kuzitaja kampuni za dawa za kulevya kama mashirika ya kigaidi.

Kadhalika, amewageukia wahamiaji wasio na vibali wanaoishi Marekani. Kupitia Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha (ICE) pamoja na Operesheni ya Utekelezaji na Uondoaji, anasema kuanzia Novemba mwaka jana, watu 1,445,549 kati yao Watanzania 301 ambao si raia wataondoshwa nchini humo.

Miongoni mwa raia wanaoondolewa ni kutoka nchi 108, wakiwamo 8,946 kutoka ukanda wa Afrika Mashariki ambao wengi ni Wasomali wanaodaiwa kufikia 4,090.

Trump anatimiza alichokiahidi kwamba atawahamisha maelfu ya wahamiaji wasio na vibali, kuondoa urasimu wa serikali, kupunguza kodi, na kuanzisha ushuru mpya kwa bidhaa za kigeni.

Kadhalika, kusitisha misaada kwenye eneo la afya na alipoingia tu ofisini alianza na kutangaza kuondoa msaada wa Wamarekani katika Shirika la Afya Duniani (WHO), ambayo ilikuwa kauli yake ya kwanza siku chache tu baada ya kutawazwa rasmi.

"Hili ni jambo kubwa," anajivuna rais huyo kutoka Chama cha Republican, muda mfupi baada ya kutia saini amri ya kuanza mchakato wa kuiondoa Marekani kuwa mwanachama wa WHO.

Marekani ilichangia dola za Marekani bilioni 1.284 katika kipindi cha 2022-2023, kuwezesha WHO. Itakumbukwa Marekani na nchi nyingine na washirika hutoa fedha ili kukabiliana na dharura, kuzuia vitisho vya magonjwa kuenea katika mipaka na kuendeleza vipaumbele vingine muhimu vya afya duniani.

**AFRIKA KUSINI**

Rais Trump ametangaza hivi karibuni pia kusitisha ufadhili kwa Afrika Kusini.

Anasema hayo Jumapili iliyopita, kwamba Afrika Kusini, ilikuwa ikinyakua ardhi na kuwanyanyasa wakulima Wazungu, huku akitangaza kupunguza ufadhili wa siku zijazo kwa nchi hiyo hadi uchunguzi ufanyike.

"Kadhalika, amewageukia wahamiaji wasio na vibali wanaoishi Marekani. Kupitia Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha (ICE) pamoja na Operesheni ya Utekelezaji na Uondoaji, anasema kuanzia Novemba mwaka jana, watu 1,445,549 kati yao Watanzania 301 ambao si raia wataondoshwa nchini humo.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, mwezi uliopita alitia saini muswada kwamba katika mazingira fulani, serikali haitatoa fidia kwa mali ambayo itaamua kuinyakua kwa maslahi ya umma.

**AIGUSA BRICS**

Trump, ameionya jumuiya ya nchi zinazoinukia kiuchumi ya BRICS, kwamba zikiacha matumizi ya Dola ya Marekani, ataziwekea ushuru wa asilimia 100.

Nchi za BRICS zinajumuisha Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (South African) zilizojiunga pamoja kutetea maslahi yake dhidi ya mifumo mingine ya kibiashara.

Anasema matumizi ya dola ya Marekani hayaepukiki na iwapo nchi hizo zitajiondoa katika matumizi hayo kama njia ya malipo yake kimataifa, atiziongezea ushuru.

Anasisitiza kuwa Marekani haiwezi kukaa kimya na kuangalia namna BRICS inavyofikiria kuachana na matumizi ya dola kama sehemu ya malipo yake kimataifa.

Rais huyo wa Marekani ameongeza kuwa iwapo nchi hizo zitachukua hatua hazitauza wala kununua bidhaa kutoka Marekani.

Jumuiya hiyo ya BRICS inazijumuiya Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini, mapema mwaka jana ilizikaribisha Iran, Misri, Ethiopia na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kujiunga huku Indonesia ikijiunga nao mwanzoni mwa mwaka huu.

BRICS iliundwa ili kukabiliana na dola, na kama mbadala wa kundi la mataifa saba yaliyoendelea kiuchumi duniani ya G7.

Rais wa Russia, Vladimir Putin amekuwa mara kwa mara akikosoa utegemezi wa dola ya Marekani na kutangaza nia yake ya kuanzisha mfumo huru wa malipo ndani ya Jumuiya ya BRICS.

China imeapa kulinda maslahi yake ya kitaifa baada ya Rais wa Marekani Donald Trump kusema kwamba ushuru wa forodha wa asilimia 10 kwa bidhaa za China unaweza kuanza kutekelezwa kuanzia Februari mosi mwaka huu.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Mao Ning, anafafanua msimamo huo akisema taifa hilo, linaamini hakuna mshindi katika vita vya kibiashara au ushuru, hivyo litaendelea kulinda maslahi yake.

Aidha, Trump anaeleza kuwa kuna haja ya kurekebisha uwiano wa kibiashara kati ya Umoja wa Ulaya na Marekani, akidai umoja huo haununui bidhaa za kutosha za Marekani na suluhisho kwa kuongeza ushuru au kuishawishi Ulaya kununua zaidi mafuta na gesi kutoka Marekani.

Wakati Rais wa Marekani anakuwa mkali kwa Afrika Kusini kwa upande mwingine sera yake kwa Afrika kwa ujumla haiko wazi.

Trump anasubiriwa kuzungumzia hatima ya Mkataba wa Ukuaji na Fursa kwa Afrika (AGOA) ambao unafikia ukingoni mwaka huu. AGOA inawezesha bidhaa za Afrika kuingizwa Marekani bila ushuru.

Kwa upande wake anataka anayenufaika 'kutojihusisha na shughuli zinazodhoofisha usalama wa Marekani au maslahi ya sera za kigeni.'"

*

**DW/BBC**



# Watanzania wakumbushwa kusaidia watu wenye uhitaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wameshauriwa kujenga utamaduni wa kusaidia watoto wenye mahitaji waliopo shuleni pamoja na wale wanaoishi kwenye vituo mbalimbali, ili kuwapunguzia changamoto wanazokutana nazo kwenye maisha yao ya kila siku.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), Godric Ngolly wakati akikabidhi misaada mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 1.5 iliyotolewa na wanafunzi wa kitengo cha itifaki ikiwa ni sehemu ya shukrani kwa kufikia miaka 45 ya chuo hicho toka kuanzishwa kwake.

Ngolly, alisema utamaduni huo wa kuwatembelea wenye mahitaji kwenye maeneo ya vituo hivyo na shuleni watapunguziwa changamoto wanazokabiliana ikiwemo za elimu afya, chakula, malazi pamoja mavazi.

Alisema kitendo hicho cha kuwatembelea na kutatua mahitaji wanayoyahitaji pia ni kuisaidia serikali na taasisi zinginezo ambazo zimekuwa na mzigo mkubwa wa kuhudumia watoto hao.

Hata hivyo, aliwataka wazazi na walezi kutowaficha ndani watoto wenye ulemavu, kwa kuwa kitendo hicho kinawaongezea umasikini mkubwa tofauti na kama wangepelekwa shule ili kupatiwa elimu.

Alisema: "Bado kuna changamoto kwa baadhi ya wazazi kama wanaamini kuwa mtoto mwenye ulemavu akisomeshwa anaweza kupata elimu ya ujuzi ambao unaweza kuwasaidia hata ndani ya familia na kuondokana na umasikini".

Katika kuadhimisha miaka hiyo ya 45 ya chuo hicho pia wanafunzi hao walishiriki kupanda miti ikiwemo ya matunda na kivuli kwenye eneo la shule hiyo ili kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mwenyekiti wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma Kitengo cha Itifaki, Rutaiwa Njoke alisema kuwa pamoja na upandaji wa miti ya matunda na kivuli wametoa misaada mbalimbali ikiwemo sabuni, mafuta, sukari, unga wa kula na ngano.

Alisema, misaada mingine ni pamoja na ndoo, sahani, vikombe, mabeseni, mchele katoni za maji, mafuta ya kupakaa, ndala, maharage, dawa za mswaki, pipi na dawa ya kuua wadudu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 1.5.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Buigiri Wasioona, Samwel Jonathan, alisema bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kulingana na aina ya wanafunzi walionao.

Alisema: "Hivyo tunawaomba wadau mbalimbali kuwakumbuka ili waweze kusoma kwa malengo ukizingatia kuwa watoto hao wana vipaji vinavyoweza kuwasaidia pindi watakapomaliza masomo yao ikiwemo kuondokana na umasikini".

# Dk. Biteko awapa mbinu za ushindi wanachama CCM

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

NAIBU Waziri Mkuu na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Dk. Doto Biteko amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kukijenga chama na kuondoa tofauti zao, ili kupata mafanikio kwenye Uchaguzi Mkuu.

Dk. Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati alitoa rai hiyo juzi kwenye hotuba yake wakati akifungua mkutano mkuu wa jimbo la Chamwino uliofanyika Kijiji cha Manchali wilayani hapa.

Hivyo, aliwataka wana CCM kuondoa tofauti zao ili kushinda kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Alisema wapinzani wao wa kisiasa wamekuwa wakipata ushindi kutokana na kura za wanachama wa CCM waliotofautiana wakati wa kura za maoni ndani ya chama.

Kadhalika, aliwataka kukisemea vizuri chama hicho kwa wananchi ili kufikisha mafanikio ya chama na serikali katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Alisema yapo mambo mengi mazuri yaliyofanywa na serikali inayoongozwa na chama hicho, hivyo ni wajibu wa wanachama hao kuyatangaza mambo mazuri kwa watu wengine.

Aliongeza kuwa kuna miradi mikubwa imetekelezwa na serikali katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo inahitaji kutangazwa ili wananchi wote waifahamu.

Alisema kwenye sekta ya afya kuna vituo vya afya, zahanati na hospitali zimejengwa katika awamu hii ya uongozi na zilizotangulia.

Kuhusu miundombinu ya barabara alisema serikali imejenga mitandao mingi ya barabara za lami na za changarawe katika mikoa yote nchini.

Mbunge wa jimbo la Chamwino na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi alisema lengo la mkutano mkuu huo ni kueleza utekelezaji wa ilani ya CCM kuanzia mwaka 2020 hadi 2025.

Ndejembi alisema kupitia wajumbe hao wananchi wengine watapata ujumbe wa maendeleo yaliyofanyika jimboni hapo.

Kadhalika, alisema maendeleo ya jimbo hilo yametokana na serikali kuwapatia fedha nyingi za miradi ya elimu, afya na miundombinu ya majengo pamoja na vifaa tiba.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Adamu Kimbisa, aliwataka wananchi wa jimbo hilo kutumia mvua zinazoendelea kunyesha kulima mazao yanayostahimili kiasi cha mvua chache zinazoendelea.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata (kulia), akimbebesha kapu lenye maandishi yanayoeleza kura za Mama Samia 2025-2030, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, wakati wa maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa kwa CCM kimkoa katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Awataka watumishi mahakama kutenda haki

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Suleiman Mwenda amewataka watumishi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba na Mkalama kuhakikisha wanafanya kazi kwa kutenda haki, ili wananchi waweze kuwa na imani na taasisi hiyo na kuendelea na maisha ya kawaida.

Alisema hayo juzi kwenye kilele cha Wiki ya Sheria nchini ambayo watumishi wa mahakama pamoja na wadau wa sheria na wananchi walishiriki.

"Katika vitabu vya dini kuna maneno yanasema kuwa haki huinua taifa, maneno hayo yanaendana na kauli mbiu yetu ya mwaka huu ambayo inasema "Umuhimu wa dhana ya haki kwa ustawi wa taifa; nafasi ya mahakama na wadau katika kuboresha mfumo jumuishi wa haki jinai,"alisema.

Mwenda alisema kutokana na hali hiyo watumishi wa mahakama wanatakiwa kuhakikisha wanatoa hukumu zinazozingatia haki kwani watu wanabugujikwa na machozi kwa kukosa haki zao katika mahakama kwa sababu zina wajibu wa kutoa haki kwa watu.

Alisema taifa litakosa ustawi, upendo na mshikamano unaoendelea utaondoka, chuki zitatawala, uvunjifu wa sheria na watu watachukua sheria mkononi kutaendelea kama mahakama hazitatoa haki kwa wananchi.

Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba na Mkalama, Luzango Khamsini aliitaka jamii kuendelea kuiamini mahakama kwani ndiyo chombo pekee kilichopewa dhamana ya kutenda haki kwa wananchi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza katika maeneo yanayotolewa elimu ya sheria katika wilaya zote mbili Iramba na Mkalama ili waendelee kuwa na ufahamu wa masuala ya sheria.



# Walimu watakiwa kutumia vishkwambi, ‘Smart phone’ wakati wa kufundisha

**Na Grace Mwakalinga,** KATAVI

WALIMU wa masomo ya sayansi na hisabati kutoka mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi, wametakiwa kutumia vishkwambi na simu za mkononi za kisasa kama nyenzo muhimu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wanapokuwa darasani.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Katavi, Silvano Sichone, wakati wa ufunguzi wa mafunzo endelevu ya walimu kazini yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda iliyopo mkoani humo.

Sichone alisema kuwa ni vyema walimu kutumia vifaa vya kisasa kama vishkwambi na simu za mkononi kwani vifaa hivyo vitawawezesha wanafunzi kupata ufahamu mzuri wa masomo yanapowasilishwa.

Aliongeza kuwa vifaa vya kidijitali kama vishkwambi na simu za mkononi vinatoa fursa ya kutoa maelezo ya kina kupitia video, picha na michoro ya kisayansi, ambayo mara nyingi ni vigumu kuonyeshwa kwa njia za kawaida, itawawezesha wanafunzi kuelewa na kukumbuka mada kwa urahisi zaidi.

Alieleza kuwa mafunzo hayo pia yatahusisha wathibiti ubora ambao wataweza kusaidia kuboresha tathmini za walimu na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mada mbalimbali za kisayansi zinazofundishwa darasani.

Mratibu wa mafunzo kutoka Katavi, Majaliwa Mkalawa, alisema washiriki 675 kutoka mikoa ya Rukwa, Songwe na Katavi wanashiriki mafunzo ya masomo ya sayansi, hisabati, pamoja na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji.

Mkalawa alifafanua kuwa walimu na wathibiti ubora, watajifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali ya kisera yanayohusiana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023.

Alisema mafunzo hayo yatajikita katika kutoa elimu inayohitajika kwa ajili ya kukabiliana na mahitaji ya sasa ya karne ya 21, ambayo inasisitiza ujuzi, ufundi na matumizi ya teknolojia.

Aliongeza kuwa mbinu mpya za ufundishaji watakazofundishwa walimu zitasaidia kuongeza hamasa kwa wanafunzi kupenda kusoma masomo hayo na kufanya vizuri kwenye mitihani.

Mwalimu wa somo la kemia, Onesmo Nasari kutoka Shule ya Sekondari Kipete iliyopo mkoani Rukwa, alisema mafunzo hayo yatamwezesha kupata mbinu mbalimbali za kufundishia ikiwamo kumudu darasa kubwa.

Mwalimu Judith Oisso, anayefundisha somo la bailojia, katika Shule ya Sekondari Myovizi iliyopo mkoani Songwe alisema, yatamsaidia kutumiza majukumu yake ipasavyo na kuongeza ufaulu.



Washtakiwa wa kesi ya mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kilolo, marehemu Christina Nindi Kibiki, wakiwa chini ya ulinzi wa askari kanzu, baada ya kufikishwa kwa mara ya nne katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa jana. Kesi hiyo, ilitajwa na kuahirishwa hadi Februari 17, mwaka huu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# TLS yalia uhaba majaji usikilizaji mashauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Mkoa wa Mbeya kimeiomba serikali kuongeza idadi ya majaji ili kuongeza kazi ya kushughulikia mashauri yanapofika mahakama ya rufani.

Aidha, kimetoa wito kwa viongozi wa siasa kuacha kupokea na kusuluhisha malalamiko kutoka kwa wananchi yanayohusu masuala ya sheria na badala yake watoe elimu kuhusu umuhimu wa kushughulikia malalamiko yao kwenye vyombo sahihi vya utoaji haki.

Mwenyekiti wa TLS Mkoa wa Mbeya, Baraka Mbwilo, alitoa wito huo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini yaliyofanyika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya.

Mbwilo alisema kumekuwapo na ucheleweshaji wa mashauri yanapofika kwenye mahakama za juu hali ambayo imesababisha baadhi yao kukata tamaa kutokana na kutopata haki zao kwa wakati waliokusudia.

Aliomba kufanyika maboresho kwenye idara ya mahakama ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Aliomba kuendelea kusogezwa kwa huduma za utoaji haki karibu na wananchi, ikiwa ni pamoja na mabaraza ya ardhi, akieleza kuwa Mkoa wa Mbeya una baraza moja la wilaya ambalo linasimamia wilaya zote huku likiwa na wenyeviti wawili pekee.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Joachim Tigana aliahidi kuwa mapendekezo yaliyotolewa na TLS yatatekelezwa na serikali, huku akidai kuwa baadhi yalishaanza kutekelezwa na serikali ili kuboresha huduma.

Alisema tayari serikali imeanza ujenzi wa mahakama katika Mkoa wa Songwe pamoja na mahakama za wilaya ili kuwasogezea huduma wananchi.

Jaji Tigana alisema serikali inaendelea kupitia na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ambazo haziendani na mahitaji ya sasa na kwamba Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya inatarajia kupunguza muda wa kushughulikia mashauri ili wananchi wapate haki zao kwa wakati.

Hivyo, aliwaomba viongozi mbalimbali wakiwamo wa dini na mila, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huduma za mahakama inayotembea, akieleza kuwa mwitikio wa wananchi kwenda kupata huduma hiyo bado ni mdogo ikilinganishwa na matarajio.

Alisema kuwa kupitia maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, wamefanikiwa kuwafikia wananchi 5,756 na kutoa elimu kuhusu masuala ya sheria na wanatumaini kwamba wananchi wengi wamepata uelewa kuhusu masuala hayo.

## Miradi ya bil.23/- kuimarisha utalii Hifadhi ya Mikumi

**Na Valentine Oforo,** Morogoro

HIFADHI ya Taifa ya Mikumi inatekeleza miradi miwili ya ujenzi wa miundombinu ya upanuzi wa uwanja wa ndege pamoja na nyumba za malazi, ili kukidhi mahitaji ya ongezeko kubwa la watalii wa ndani na nje ya nchi.

Miradi hiyo ambayo inatekelezwa kwa Sh.bilioni 23 ikiwa ni fedha za Benki ya Dunia (WB) kupitia mradi wa kuendeleza maliasili na kukuza utalii RE-GROW, huku kukiwa na ushirikishwaji wa sekta binafsi hususani kwenye eneo la kuwekeza katika huduma za malazi.

Kwa sasa Hifadhi ya Mikumi ambayo ni ya nne kwa ukubwa nchini Tanzania inapokea zaidi ya wageni 1,000 kwa siku, ongezeko linaloshuhudia wazawa wengi wakitembelea hifadhi hiyo.

Ofisa Mhifadhi Daraja la Pili, Zamzam Yusuph, alisema katika kuanzia Julai 2024 hadi sasa hifadhi imefanikiwa kukusanya asilimia 89 ya mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa mwaka huu, ambayo ni zaidi ya Sh. bilioni 6.8.

“Rekodi zetu zinaonyesha kuwa jumla ya wageni wapatao 115,009, kutoka ndani na nje ya nchi, walitembelea hifadhi katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Januari 30, 2025, na kutuwezesha kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 6.4, alisema.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi Augustine Massesa alisema kuanza kufanya kazi kwa mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma kumetoa mchango mkubwa katika ongezeko la watalii wa ndani na nje wanaotembelea hifadhi hiyo inayopatikana Mkoa wa Morogoro.





# ZRA yakusanya bil.81/- Januari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Kamishna Mkuu wa Mamkala ya Mapato Zanzibar (ZRA), Said Ali Mohammed amesema mamlaka hiyo imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 81.512 kwa kipindi cha Januari mwaka huu.

Makusanyo hayo ni ufanisi wa asilimia 100.65 ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa kwa kipindi hicho cha Sh. bilioni 80.9.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini, alisema makusanyo ya Januari mwaka 2024 yalikuwa ni Sh. bilioni 70.180 yakilinganishwa na makusanyo ya Januari mwaka huu ambayo yameonesha ongezeko la Sh. bilioni 11.332.

Aidha, alisema ukusanyaji huo ni wa kihistoria katika ukusanyaji wa mapato ambayo yamewahi kukusanywa na ZRA.

**Pia ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 510.545 ambao ni ufanisi wa asilimia 102.07 wa makusanyo ya mapato yaliyokadiriwa katika kipindi hicho.**

Said alisema kuwa hali ya makusanyo kwa kipindi cha miezi saba kuanzia Julai hadi Januari kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ZRA ilikadiriwa kukusanya Sh. bilioni 500.187.

Alisema pia ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 510.545 ambao ni ufanisi wa asilimia 102.07 wa makusanyo ya mapato yaliyokadiriwa katika kipindi hicho.

Hata hivyo alisema kwa kulinganisha na makusanyo ya Julai hadi Januari ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa ni Sh. bilioni 421.949 ambayo yameonesha ongezeko la makusanyo ya Sh.bilioni 88.595 sawa na ukuaji wa makusanyo ya asilimia 21.00.

Akizungumzia sababu zilizosababisha kufanya vizuri kwa mwezi huo alisema ni juhudi zinazofanywa na viongozi wakuu wa nchi kwa kuweka mazingira bora yanayovutia uwekezaji unaoendelea Zanzibar.

"Mazingira bora ni pamoja na kuimarisha amani umoja na mshikamano na sera za kodi zinazotabirika na ndiyo maana uwekezaji mkubwa unaofanyika na unachangia ukusanyaji wa mapato ya serikali," alisema.

Alitaja sababu nyingine ni kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, kuongezeka kwa matumizi ya mafuta ya nishati kwa vyombo vya moto vya barabarani na kuimarika kwa uzuwiaji wa kodi.

Alisema kuwa kwa madhumuni ya kuendelea na hatua za ukusanyaji katika kipindi cha Februari 2025 mwaka wa fedha 2024/2025 ZRA itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuendelea kufanya vizuri katika kusimamia jukumu hilo.

Alisema mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu ya kodi kwa makundi mbalimbali ya walipakodi na wananchi ili kutoa uelewa wa masuala ya kodi ikiwamo matumizi sahihi ya mifumo ya kodi.

Alisema kuwa mikakati mingine ni kuendelea na mazoezi maalumu ya ufuatiliaji wa walipakodi ili kuwashajihisha matumizi sahihi ya mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki na kuweka kambi maalumu za kodi kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma karibu.

Sambamba na hayo, alisema kuimarisha ukaguzi na ufuatiliaji wa mizigo inayoingizwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara kupitia Bandari za Zanzibar na kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa miradi yote ya serikali ambayo ujenzi wake unaendelea ili kufahamu na kukusanya kiwango sahihi cha kodi kupitia miradi hiyo.

## Wajasiriamali 100 kupewa elimu ya fedha na masoko

**Na Pilly Kigome**

WAJASIRIAMALI wadogo 100 kutoka vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanatarajiwa kujengewa uwezo wa elimu ya fedha ili waweze kuzalisha ajira na kuchangia pato la taifa nchini.

Vilevile, watapatiwa elimu ya teknolojia ya biashara, masoko pamoja na kupewa mikopo.

Wajasiriamali hao watafikiwa kutokana na kuingia kwa makubaliano kati ya Shirika Huru la Kuwajengea Uwezo Asasi za Kiraia (FCS) kwa ushirikiano na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).


Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mtendaji (FCS), Justice Rutenge alisema mchakato wa kuwapata wajasiriamali hao utafuata mtitiriko ili kuwafikia walengwa ikiwamo kwenda kwenye vyama vya wenye ulemavu kama vile SHIVYAWATA, makundi ya vijana na wanawake wajasiriamali ili kuchukua watu sahihi ambao watakaokwenda kunufaika.

Alisema mchakato huo utakuwa ni wa kujaza maombi na kisha kuchuja majina ambao watakwenda kunufaika na mafunzo kwa gharama ambazo zitatolewa na SIDO na FCS.

Alisema walengwa watachangia kiasi kidogo ikiwamo nauli za kuwafikisha sehemu ya mafunzo.

Rutenge alisema mafunzo hayo yatakwenda kuwainua na kuwajengea uwezo katika kupanua elimu ya biashara ikiwamo kuzalisha ajira kwa makundi hayo.

Meneja wa Mkoa wa Dar es Salaam wa SIDO, Hopeness Elia, alisema shirika hilo litatoa mafunzo ya wajasiriamali hao jinsi ya kuendesha biashara, kurasimisha biashara zao ili kutoka hatua moja kwenda nyingine ili kupanua biashara zao.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya siku mbili kwa watendaji wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mkoani Tanga, wakifanya mafunzo kwa vitendo ya namna ya kuendesha vifaa vya Biometriki (BVR) jana, vitakavyotumika katika zoezi hilo, linalotarajiwa mkoani humo kuanza Februari 13 hadi 19, mwaka huu. **PICHA: INEC**

## Wahimizwa kutoa barua wadhamini wa watuhumiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mzee Ali Mzee, amewataka masheha kushirikiana na jamii kutoa barua za wadhamini wa watuhumiwa wanaofikishwa katika vyombo vya sheria, ili kurahisisha mchakato wa upatikanaji haki mahakamani.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua Kongamano la Wiki ya Sheria Zanzibar lenye lengo la kuhamasisha jamii juu ya masuala yanayohusu haki na sheria.

Alisema watuhumiwa wa kesi nyingi hukosa dhamana kutokana na kukosekana kwa barua za sheha kwa wadhamini jambo ambalo ni miongoni mwa masharti yaliyowekwa, hivyo kuwanyima amani washtakiwa.

Alisema kuwa masheha wana jukumu kubwa na kuhakikisha hawawi kikwazo cha watuhumiwa kupata dhamana kwenye makosa yanayodhaminika, hivyo aliwataka kujitahidi kutimiza majukumu yao.

Aidha, alisema Wiki ya Sheria ni muhimu na mahakama inafanya jambo kubwa katika kuadhimisha ikiwa inaashiria kuanza kwa mwaka mpya wa 2025.

Alisema kuwapo kwa wiki hiyo itawatoa hofu jamii na kuweza kuiamini mahakama pale inaposimamia haki na wajibu wa kila mtu katika kupata haki yake kwa mujibu wa sheria.

"Mahakama ni chombo kinachohakikisha sheria inafuatwa na kutafuta haki na siyo sehemu ya kutia hofu, hivyo ni vyema jamii kuelimishwa kwamba dhamira ya chombo hicho kutoa haki kwa wananchi katika kutoa mfumo wa haki jinai," alisema.

Alisema kuna taasisi mbalimbali zina nafasi kubwa ya kutoa taaluma kwa jamii ikiwamo polisi katika eneo la upelelezi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na mahakama ndio inayofanya uamuzi.

Alisema kesi nyingi zinazoripotiwa mahakamani ni za dawa za kulevya, udhalilishaji na rushwa makosa ambayo yamekithiri zaidi.

Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Khamis Rashid Khamis, alisema wataendelea kuhakikisha mahakama inasimamia utoaji wa haki kwa wananchi ili haki itendeke.

Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Othman Ame Chum, alisema wiki hiyo ni kuimarisha utendaji wa mahakama katika kusimamia wananchi ili kutoa haki za migogoro ya ndoa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**THECKLA XAVERY KAYOMBO** anatangaza kupotelewa na cheti Cha kidato Cha nne chenye index namba **S1197/0078** kilichotolewa na **Green Acres Sec School** mwaka 2014. Cheti Cha Chuo Higher Diploma in International Relations and Diplomacy (CFR) chenye namba **CFR/NTA7/258** kilichotolewa na Centre for Foreign Relations (CFR) mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/9367/2025.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KIBIBI ABDALLAH MWINYI MANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye index namba **PS.0203018/132** kilichotolewa na Shule ya Msingi Kawe mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/9692/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**NICE SHAABAN MKWEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 262 DMV - BAJAJ BOXER.** Kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 972 DJW – BAJAJ BOXER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/18858/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA BAJAJI

**PATRICK MAKENE KAJIJI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 857 BBW – TOYOTA COROLLA.** Kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 476 BWQ.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/19955/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JAMES MUSAFIRI KIHWELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA **TVS KING** YENYE USAJILI **MC 629ECX** RANGI YA KIJANI, KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA YA POLISI: **PHQ/IRI/IRI/1614/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LUCTON RUGARABAMU FRANCES,** Anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki aina ya sunlg zenye namba za usajili **mc 807ajt** na **mc 906 dgj.** Yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/KAG/KYE/1452/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANGETILE ASELI MWANGATA,** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 482 DEK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chaochote cha Polisi kilichopo jirani yake Taarifa ya Polisi **PHQ/MBE/MBE/2960/2025**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA SHINYANGA**
**RUFAA YA JINAI NA.30582/2024**
**(ASILIA SHAURI LA JINAI NA.2076 YA 2024 KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA SHINYANGA)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA**
**DHIDI YA**
**EVANS MAIGE@GATINGA**
**TYSON MAINA@WANGOI**
**STEVEN ADENYA@MISE**

**KWA: EVANS MAIGE@GATINGA**
**TYSON MAINA@WANGOI**
**STEVEN ADENYA@MISE**

**TAARIFA YA KUITWA SHAURINI**

Mnajulishwa kwamba mnamo tarehe 17/2/2025 saa 4:00 asubuhi shauri tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa.
Hivyo mnaamriwa kuhudhuria siku hiyo mbele ya Mahakama Kuu Shinyanga bila kukosa.
Endapo hamtahudhuria rufaa hiyo itasikilizwa na kutolewa uamuzi bila nyinyi kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama leo tarehe 11/12/2024

A.H. MWETINDWA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.08/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HALIMA MZINZI wa MJIMPYA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAREHE YUSUPH HAJI**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 02 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 28 Mwezi 01 Mwaka 2025.

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1900 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LUSAJO AKIM MWAIPYANA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

**GWANDUMI MALAMULA MWAIPYANA….1ST PETITIONER**

**ATUPAKISYE AIZACK PANJA…………..2ND PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of February, 2025.
Dated at KYELA MBEYA this 30 day of January, 2025.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya SINGIDA**

**Kituo cha UTEMINI Mkoa wa SINGIDA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 10/2025**

**Jina la Mdai: MWANAIDI JUMANNE MKOKO**

**Jina la Mdaiwa: OMARI HAMISI MUGHENYI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za utaratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: OMARI HAMISI MUGHENYI**

**K.K MWENYEKITI WA MTAA WA STATION**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TALAKA CHUMO LA PAMOJA NA MATUNZO YA WATOTO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 14 Mwezi 02 Mwaka 2025 saa 3:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
UTEMINI

---

**Land Disputes Courts (The District Land and Housing Tribunal) Regulations GN. No 174/2003**

**Form No 2B**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KASULU**
**MAHALI: KASULU**

**MAOMBI NA…………142…………MWAKA ………………2024**

**MFAUME MZEE KAKUYA……………………………..MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PIUS SIMON, ITUMBO NYACHARO, FIKIRI SAID, BAHATI MATONE, MWANA MAMINGULA, OMARY WILLIAM ……………MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**PIUS SIMON, ITUMBO NYACHARO, FIKIRI SAID, BAHATI MATONE, MWANA OMARY…MJIBU MAOMBI**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 27…Mwezi 02……2025 …Saa 02:30 Asubuhi mbele ya mheshimiwa MOURICE Mwenyekiti wa Braza, hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu Lakiri/Muhuriwa Baraza hili leo tarehe 20….Mwezi …01…Mwaka…….2025.

MWENYEKITI

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watu 900 wauawa DRC, M23 ikisitisha mapigano

## • EAC, SADC kukutana Dar Jumamosi

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema takribani watu 900 wameuawa na wengine 2,900 kujeruhiwa kutokana na mapigano yaliyodumu kwa siku saba katika mji wa Goma kati ya waasi wa M23 na Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Shirika la Uratibu wa Misaada ya Kiutu la Umoja wa Mataifa (OCHA) linasema, idadi hiyo ya watu 900 iliyotolewa na WHO katika ripoti yake, haijumuishi miili ya watu waliouawa kutokana na vita hivyo, ambayo iko kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti.

Inaelezwa kuwa miili ya watu bado imetapakaa katika mitaa ya mji wa Goma. Huku waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda wakitangaza kusitisha mapigano hayo kuanzia jana ili kuruhusu misaada ya kibinadamu kuingia katika mji wa Goma ulioshuhudia machafuko makali.

Wakati hayo yakijiri Rais wa Rwanda, Paul Kagame na Rais wa DRC, Félix Tshisekedi wanatarajiwa kushiriki katika mkutano wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) Februari 8, mwaka huu jijini Dar es Salaam, ili kujadili mzozo huo.

Inaelezwa kuwa hatua ya M23 kusitisha mapigano inafuatia miito ya jumuiya hizo ili kuruhusu misaada ya kibinadamu kutolewa kwa maelfu ya watu walioachwa bila makazi katika mji wa Goma wenye wakazi takribani milioni tatu, huku milioni moja wakiwa wamekimbia makazi yao.

Usitishaji huo mapigano unajiri pia kuelekea mkutano wa kilele wa pamoja wa EAC na SADC wiki hii ambako Rais wa Kenya William Ruto amethibitisha kwamba Rais Kagame na Tshisekedi watahudhuria.

Inaelezwa kuwa viongozi hao wote wawili wamekuwa wakikwepa kuhudhuria mikutano ya awali ya kutafuta amani katika mzozo unaoendelea nchini Kongo.

Mamlaka nchini Kongo zinasema ziko tayari kwa mazungumzo ya kuleta amani ila mazungumzo hayo ni sharti yafanyike kwa muktadha wa makubaliano yaliyopita.

Waasi hao wanadaiwa sasa kuelekea katika mji wa Bukavu



Maofisa wa Shirika la Msalaba Mwekundu wakisitiri na kupakia miili ya watu waliouawa kwenye mapigano katika mji wa Goma. **PICHA: MTANDAO**

> Mmoja wa wakazi muuza duka katika mji wa Goma Sammy Matabishi anasema "Watu wanauoga...bado nina hofu kwasababu wale walioleta vurugu bado wako miongoni mwetu na hatujui kinachoendelea kwa sasa."

ingawa Jumatatu walithibitisha kwamba hawana nia ya kuuteka mji huo, huku wakisema awali kwamba wanapania kwenda katika Mji Mkuu Kinshasa.

**KUHUSU MKUTANO**

Rais Ruto ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki EAC anasema mkutano wa jumuiya hizo unaotarajiwa kufanyika wiki hii nchini, umekuja baada ya viongozi wa jumuiya kwa nyakati tofauti kukubaliana kuwa na mkutano wa pamoja.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa endapo Rais Kagame na Rais Tshisekedi watahudhuria mkutano huo kama inavyotarajiwa itakuwa ni mara ya kwanza kukutana ana kwa ana tangu kundi la M23 lichukue mji wa Goma.

Katika kikao cha wakuu wa nchi za Afrika Mashariki kilichofanyika juma moja lililopita kwa njia ya mtandao, Rais Tshisekedi hakuhudhuria uamuzi ulioibua maswali ikiwa yuko tayari kwa mazungumzo ya kusaka suluhu ya kudumu kati yake na Rwanda.

Wataalamu wanaeleza kuwa mkutano huo wa wiki hii utakuwa wa muhimu hasa ikizingatia yanayoendelea kutokea na ambayo yanatishia usalama wa kikanda na kwamba ni lazima wakuu hao wa nchi watoke na azimio litakalosaidia kupatikana kwa suluhu ya kudumu.

Mji wa Goma uko katikati ya eneo lenye utajiri wa madini ikiwemo shaba, cobalt, dhahabu na coltan yanayotumika kutengeneza simu za rununu na betri za magari ya umeme, unasalia kuwa chini ya udhibiti wa waasi wa M23 wanaoripotiwa kusonga mbele na kuchukua udhibiti wa maeneo mengine ya mashariki mwa DRC.

**HALI ILIVYO**

Inaelezwa kuwa kwa sasa, Goma ndio mji ambao M23 wanajivunia kuuteka. Huku hali ya eneo hilo ikionyesha taswira vile hali itakavyokuwa iwapo waasi hao wataendelea kuteka na kudhibiti miji mingine zaidi.

Kadhalika inaelezwa kuwa wengi wa wananchi wanasema wameanza kuzoea kutawaliwa na kundi la M23.

Vile vile, taarifa zinaeleza kuwa waasi hao walifanikiwa kudhibiti hadi ofisi ya Gavana wa kijeshi wa Kivu Kaskazini, ambaye walimuua walipokuwa wakiingia na kuvamia mji wa Goma.

Pia inabainishwa kuwa wapiganaji walikuwa wakishika doria katika maeneo mbalimbali katika eneo hilo, huku wengine wakizunguka mjini wakiwa wamebeba silaha.

Kutokana na hali hiyo inaelezwa kuwa watu wengi bado wana wasiwasi wakihofia uwezekano wa kurejea kwa mapigano katika mkoa wa Kivu Kaskazini.

Mmoja wa wakazi muuza duka katika mji wa Goma Sammy Matabishi anasema "Watu wanauoga...bado nina hofu kwasababu wale walioleta vurugu bado wako miongoni mwetu na hatujui kinachoendelea kwa sasa."

"Lakini cha kushangaza zaidi ni kuwa hakuna anayekuja kununua bidhaa madukani mwetu, wengi wamehamia Rwanda, mji ulioko mpakani na Kongo Bukavu, Kenya na Uganda," anasema

Wakati huo, M23 wakisherehekea ushindi mkubwa licha ya kutangaza kusitisha mapigano, serikali ya Kongo inaendelea kukataa madai kwamba waasi hao wameuteka kikamilifu mji wa Goma.

Mamlaka ya DRC imekuwa ikiwashutumu M23 kwa kuchukua ardhi yao kinyume cha sheria kwa madai ya kupatiwa msaada na Rwanda, huku ikiahidi kurejesha maeneo yaliyopotea.

Ingawa Rwanda imekuwa ikikanusha mara kwa mara kuhusika na kuunga mkono waasi wa M23, majibu yake yameanza kugeuka na kuwa ya kujitetea, huku msemaji wa serikali hiyo akieleza kuwa vita vinavyoshuhudiwa karibu na mpaka wao ni tishio kwa usalama wao.

Waasi sasa wanadaiwa kusogea kusini kuelekea Bukavu, mji mkuu wa Kivu Kaskazini, na wameapa kufika katika mji mkuu wa nchi hiyo, Kinshasa.

**UNYANYASAJI**

Wakati mashariki mwa Kongo inakumbwa na misukosuko ya kisiasa, Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa inatahadharisha kuwa unyanyasaji wa kijinsia unatumika kama silaha ya vita na pande pinzani.

Daktari katika moja ya hospitali binafsi katika eneo hilo alithibitisha kauli ya Umoja wa Mataifa, akisema taasisi yake imepokea hadi sasa waathiriwa 10 wa ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia.

Inaelezwa kuwa ingawa milio ya risasi na milipuko mjini Goma imepungua, sio maeneo yote ambayo shughuli za kila siku zimerejea kama kawaida.

# MOROCCO AKUNWA UWEZO WA DIARRA WA YANGA SC

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Timu ya Taifa ' Taifa Stars', Hemed Suleiman 'Morocco' amesema katika wachezaji wa nje wanaocheza soka la kulipwa hapa nchini, anavutiwa zaidi na golikipa wa Yanga, Djigui Diarra na kama angekuwa Mtanzania angeisaidia sana Stars.

Morocco akihojiwa katika kituo kimoja cha luninga jijini Dar es Salaam juzi usiku, alisema Diara ni golikipa aliyekamilika na anaweza kuituliza na kuiongoza vizuri timu uwanjani.

"Kwa wachezaji wa nje wanaocheza hapa nchini, kwangu mimi Diarra wa Yanga, kama angekuwa Mtanzania angetusaidia sana, unajua hakuna eneo muhimu kwenye timu kama la golikipa, ni mchezaji mzuri na amekamilika," alisema Morocco.

Alisema kumtaja Diarra kama mchezaji wake bora wa kigeni wanaocheza soka la kulipwa hapa nchini, haimaanishi hakuna wachezaji wengine wazuri zaidi.

"Kuna wachezaji wengi wazuri sana ambao wapo kwenye ligi yetu wakitoka nchi mbalimbali, lakini kwa umuhimu wa nafasi na aina ya uchezaji wake, Diarra ni mchezaji aliyekamilika sana kwenye nafasi yake, timu yoyote ya taifa inahitaji uimara wa mlinda mlango.

"Hata ukiangalia pale Yanga ni mchezaji tegemeo, amekuwa chachu ya mafanikio ya klabu yake, namna anavyoanzisha mashambulizi, namna anavyowapanga mabeki wake...., yuko vizuri kwa kweli," alisema Morocco ambaye Desemba mwaka huu ataiongoza Stars kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2025, akiwa kocha Mkuu wa timu hiyo.

Taifa Stars mwaka huu itashiriki fainali hizo kwa mara ya pili mfululizo huku pia zikiwa fainali zake za nne kushiriki kwa ujumla wake.



Mshindi namba moja wa mchezo wa Vishada, Omar Abdallah (katikati), akionesha kombe alilotwaa sambamba na mshindi wa pili, Khamis Suleiman (kulia) na Mfaransa Hugo Beaomont, aliyeshika nafasi ya tatu katika mashindano hayo yaliyofanyika Jumatatu katika Pwani ya Kiwengwa, Zanzibar. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Wazanzibar wang'ara vishada kimataifa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WACHEZAJI wa mchezo wa Kurusha Vishada Baharini kutoka Zanzibar wameng'ara katika michuano ya kimataifa ya mchezo huo iliyofanyika juzi, Jumatatu katika Pwani ya Kiwengwa na kushirikisha jumla ya nchi nane.

Zanzibar imefanikiwa kutoa mshindi wa kwanza ambaye ni Omar Abdallah, aliyezawadiwa medali na kombe pamoja na kitita cha Dola za Marekani 3,000 huku nafasi ya pili ikichukuliwa na Khamis Suleiman ambaye alizawadiwa Dola 2,000, wakati nafasi ya tatu ikichukuliwa na Raia wa Ufaransa, Hugo Beaomont, aliyezawadiwa Dola 1,000.

Nafasi ya nne ilikwenda kwa Fadhil Pandu, aliyezawadiwa Dola 200, wakati mshindi wa tano Khamis Haji alizawadiwa Dola 50, wote wakiwa ni kutoka Zanzibar isipokuwa Mfaransa huyo aliyeshika nafasi ya tatu.

Akizungumza katika hafla ya fainali ya mashindano hayo juzi, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ), Said Marin, alisema Zanzibar imejipanga katika kuimarisha utalii wa michezo ili kuongeza idadi ya wageni wanaotembelea hapa nchini.

Alisema katika mashindano hayo ya kimataifa wageni mbalimbali wameshiriki ikiwamo kutoka Ufaransa, Italia na nchi nyingi za nje, hivyo ni dhahiri kuwa mchezo huo umekuwa na thamani kubwa kwa kuitangaza Zanzibar kimataifa.

"Tunaamini mchezo huu wa leo umeipa sifa sana Zanzibar katika anga za kimataifa na ndio lengo letu," alisema.

Marin alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia baraza lake la michezo imejipanga kuhakikisha kuwa michezo yote inaimarika ili kutoa nafasi kwa wachezaji wa ndani kuendelea kushindana katika sekta hiyo.

Aidha, katibu huyo alisema kuwa vijana Wakizanzibari, wameonesha ukomavu katika mchezo huo na kushika nafasi ya kwanza na ya pili.

Naye Mkurugenzi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Adili George, alisema malengo ya mchezo huo wa kimataifa wa vishada ni kuendelea kuitangaza Zanzibar katika sekta ya utalii kwenye mandhari nzuri ya bahari.

Alisema Kamisheni ya Utalii imejipanga katika kuendeleza mchezo huo kwa vijana wote hapa nchini ili kupata fursa ya kushindana katika mashindano mengine ya kimataifa.

Kwa upande wa mshindi wa mashindano hayo, Omar Abdallah, alisema vijana wengi wanauwezo wa kushindana katika mashindano hayo, lakini tatizo kubwa uwezeshwaji umekuwa changamoto.

Alisema ushindi huo alioupata kwa upande wake umempa faraja kwa vile amepata nafasi ya kushiriki na washiriki kutoka mataifa mengine na kupata uzoefu zaidi.

## Simba yaliteka Bunge Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TIMU ya soka ya Simba ambayo imefuzu robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu, imetinga bungeni na kushangiliwa na wabunge baada ya Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, kutangaza uwapo wao mjengoni.

Simba ambayo ni klabu pekee ya Tanzania inayoiwakilisha kwenye michuano ya kimataifa, wachezaji, benchi la ufundi na menejimenti ya klabu hiyo walitambulishwa jana bungeni katika kipindi cha maswali na majibu na Zungu.

Akiwatambulisha Naibu Spika Zungu, alisema "Kwa taarifa ya kipekee kwa mujibu wa mitandao ya kijamii Simba ni klabu pekee iliyopo kwenye michuano inayosimamiwa na CAF, Mheshimiwa Tarimba mbona umekasirika? Michuano inasimamiwa na CAF kwa Ukanda wa Afrika na ndio klabu pekee ya Tanzania inayoshiriki robo fainali kwa mara ya sita mfululizo."

Alisema pamoja na Simba kuna Klabu ya Yanga ambayo ni timu muhimu kwa umoja wa taifa na kwamba namna Yanga na Simba zinavyoitangaza Tanzania inampa sifa sana Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tanzania inakuwa kwenye ramani ya Afrika na Dunia kwa klabu hizi mbili muhimu kwa taifa letu,"alisema.

## Mwenge kutofanya makosa tena Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mwenge SC imesema itahakikisha haifanyi makosa yoyote ya kupoteza alama tatu katika michezo yao ya ugenini ambayo watacheza Unguja.

Mwenge SC bado ipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja kutokana na kuwa na pointi 19 zinazoiweka nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omar Khamis 'Matu' alisema anajua ligi hiyo ina ushindani mkubwa hasa katika mzunguko huu wa mwisho, lakini amejipanga kukabiliana na vishindo vyote.

Alisema kushinda mchezo wake wa kwanza katika mzunguko huu wa lala salama kunaendelea kumpa ari na nguvu ya kushinda michezo mingine.

"Ligi bado ni ngumu sana, kila mmoja yupo kuhakikisha anatimiza mipango yake aliyojipangia, kuna wanaoutaka ubingwa na wale ambao wanahitaji kubaki Ligi Kuu" alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RASHFORD BASI TENA UNITED

MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, ambaye amejiunga na Klabu ya Aston Villa kwa mkopo, huenda asicheze tena Manchester United kwa vile uhusiano kati ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na timu hiyo ya Old Trafford umesambaratika. (***Guardian***)

### KLUIVERT ATAJWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inajiandaa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth na Uholanzi, Justin Kluivert mwenye umri wa miaka 25, kama msimu wa majira ya joto itampoteza Alexander Isak, 25. (***Sun***)

### GUEHI AWA LULU EPL

NEWCASTLE United na Tottenham Hotspur huenda zikafufua nia ya kumsajili mlinzi wa Crystal Palace, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, msimu wa majira ya joto atakapoingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake, baada ya Spurs kukataliwa ofa yao mwishoni mwa dirisha la Januari. ***(Sky Sports)***

### WILLIAMS ATAKIWA ARSENAL

WINGA wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, ni kipaumbele cha usajili wa Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta. (***Football transfer***)

### JORGINHO SAFI FLAMENGO

KIUNGO wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 33, ametia saini makubaliano ya awali ya mkataba wa kujiunga na Flamengo ya Brazil msimu ujao wakati mkataba wake na 'washikabunduki' utakapokamilika. (***Mirror***)

### CONTE ALIA KUMKOSA GARNACHO

KOCHA wa Napoli, Antonio Conte, amesikitishwa na hatua ya klabu hiyo kutomsajili winga wa Manchester United na Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20, au mshambuliaji wa Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye miaka 23, kutoka Borussia Dortmund, katika dirisha la Januari baada ya kumuuza winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia (23), kwa Paris St-Germain. (***Sky Sports Italia***)

### NKUNKU NA UNITED, BAYERN

KLABU ya Manchester United na Bayern Munich zote zilimtaka mshambuliaji wa Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27 katika dirisha la Januari. ***(Mail)***

### ARSENAL PATUPU JANUARI

ARSENAL haikumsajili mchezaji yeyote katika uhamisho wa Januari, lakini mikataba ya mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 21 na kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye miaka 26, huenda ikaongezwa. ***(Football.London)***

### TRUFFERT NA EVERTON

KLABU ya Everton inashughulikia mpango wa kumsajili beki wa kushoto wa Rennes na Ufaransa, Adrien Truffert, 23. ***(Mail)***

### GLASNER AMTAKA PAVLOVIC

KOCHA wa Crystal Palace, Oliver Glasner, anataka kumsajili kiungo wa AC Milan na Serbia, Strahinja Pavlovic mwenye umri wa miaka 23, kwa mkataba wa pauni milioni 25. (***Sun***)

### KROUPI AFIKIRIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Lorient, Eli Junior Kroupi mwenye umri wa miaka 18, ambaye pia anawindwa na Chelsea na West Ham. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# RONALDO AFIKISHA USHINDI MECHI 700 NGAZI YA KLABU

**RIYADH,** Saudi Arabia

**Pia ametupia jumla ya mabao 923, huku mafanikio yake makubwa akiyapata akiwa...**

CRISTIANO Ronaldo amesherehekea ushindi wake wa 700 kwa ngazi ya klabu katika maisha yake ya soka kwa kufunga mabao mawili wakati akiiongoza Al Nassr kushinda 4-0 dhidi ya Al Wasl ya Iran kwenye Ligi ya Mabingwa Asia Jumatatu usiku.

**Ushindi huo umekuja siku mbili tu kabla ya fowadi huyo wa Ureno kusherehekea kutimiza umri wa miaka 40 ya kuzaliwa kwake.**

Nahodha huyo wa Al Nassr alianza kufunga kwa penalti huku timu yake ikishinda mara nne mfululizo katika mashindano yote na kufuzu kuingia hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Asia.

Huo ulikuwa ni ushindi wa 66 kwa Ronaldo akiwa na Al Nassr tangu ajiunge na klabu hiyo ya Saudia Desemba 2022 baada ya kukatiza mkataba wake na Manchester United.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, alianza soka lake la kulipwa Agosti 2002.

Ronaldo alishinda michezo 13 akiwa na Sporting CP kabla ya kuwasili Old Trafford mwaka 2003 na kushinda mechi 214 katika vipindi viwili akiwa na United, akifunga mabao 145 katika mechi 346.

Real Madrid ndipo ambapo Ronaldo alipata mafanikio yake mengi kwani alishinda mara 315 akiwa na 'Los Blancos' hao na kunyanyua mataji 15, yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo alishinda mechi 92 akiwa na Juventus katika misimu mitatu kabla ya kurejea Manchester United Agosti 2021.

Mshambuliaji wa Inter Miami ya Marekani, Lionel Messi, ameshinda michezo 613 katika ngazi ya klabu, ikijumuisha 542 akiwa na Barcelona.

Ronaldo alikuwa amefunga mabao 921 kufikia Januari 30, huku mabao yake hayo mawili sasa yakimfanya kufikisha jumla ya mabao 923 katika maisha yake ya soka.

Nahodha huyo wa Ureno pia anashikilia rekodi ya dunia ya wanaume kwa kufunga mabao mengi ya kimataifa akiwa na mabao 135.

# MAN CITY YAMTWAA RASMI GONZALEZ



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imekamilisha usajili wa Nicolas Gonzalez kutoka FC Porto katika siku ya mwisho juzi.

ESPN iliripoti mapema Jumatatu kwamba timu hizo mbili zilikuwa kwenye mazungumzo juu ya hatima yake na klabu hiyo ya Ligi Kuu England hazikuweka wazi kitita kilichotolewa kwa ada ya mchezaji huyo, lakini inaaminika kwamba ni euro milioni 60.

Ametia saini mkataba utakaomalizika 2029 na inadaiwa Porto haikuwa tayari kupunguza thamani ya mchezaji huyo kwa sababu sehemu ya malipo itapewa klabu yake ya zamani ya Gonzalez, Barcelona.

Raia huyo wa Hispania alihamia Ureno kutoka LaLiga mwaka 2023 na chanzo kimeiambia ESPN kwamba malipo yanayodaiwa na Barcelona iwapo Gonzalez atahama yanaweza kuwa ya juu hadi asilimia 40 ya ada yote ya uhamisho.

"Hii ni fursa nzuri kwangu katika hatua hii ya uchezaji wangu," alisema Gonzalez.

"Nina umri wa miaka 23, na ninataka kujjaribu Uingereza. Hakuna klabu bora zaidi kuliko Manchester City kwangu kufanya hivyo.

"Angalia kikosi walichonacho hapa, kimejaa wachezaji wa kiwango cha kimataifa. Hakuna mwanasoka duniani ambaye hangependa kuwa sehemu ya timu hii.

"Najua sifa aliyonayo kocha Pep Guardiola na siwezi kusubiri kufanya kazi naye. Kwa kweli, nina heshima, anataka nicheze katika timu yake.

"Nimefurahi sana. Nataka tu kukutana na wachezaji wenzangu, na wafanyakazi wa hapa na kucheza mbele ya mashabiki wa City!"

Uhamisho huo unachukua matumizi ya City Januari hadi karibu euro milioni 210 baada ya ununuzi wa Omar Marmoush, Abdukodir Khusanov na Vitor Reis pamoja na Gonzalez.

# Chelsea yamtoa Chilwell kwa Palace

**LONDON,** England

KLABU ya Crystal Palace imemsajili rasmi Ben Chilwell aliyeondoka Chelsea kwa mkataba wa mkopo kwa muda uliosalia wa msimu huu.

Kocha Enzo Maresca aliweka wazi kuwa hakuna nafasi kwenye kikosi chake kwa Chilwell mwanzoni mwa msimu huu.

Muitaliano huyo ametimiza neno lake, na kumpa beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 28, jumla ya dakika 45 katika mashindano yote.

Chilwell hakuonekana hata katika mojawapo ya kikosi cha siku ya mechi cha Ligi Kuu ya klabu hiyo, achilia mbali kuingia uwanjani.

Palace wamekubali mkopo wa miezi sita kwa Chilwell, ambaye bado ana mkataba Chelsea hadi Juni 2027.

Kutokana na jeraha la mwisho la msimu kwa Chadi Riad, Tyrick Mitchell alikuwa beki pekee wa kushoto wa Palace kabla ya kuwasili kwa Chilwell.

Chilwell hajaanza mechi yoyote ya Ligi Kuu England tangu awe nahodha wa Chelsea na kutoka sare ya mabao 2-2 na Brentford Jumamosi ya kwanza ya Machi 2024 - zaidi ya miezi 11 iliyopita.




# Spurs yazipiku Arsenal, Chelsea kumtwaa Tel

**LONDON,** England

TOTTENHAM Hotspur imezipiku Arsenal, Chelsea na Manchester United kumsajili mshambuliaji chipukizi wa Bayern Munich, Mathys Tel kwa mkopo na bila kipengele cha kumnunua jumla.

Ilibainika kuwa Tel alikuwa na nia ya kuondoka Bayern mwishoni mwa Januari huku akitafuta muda zaidi wa kucheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ameanza mechi nne pekee katika michuano yote msimu huu huku akicheza mechi kumi zaidi akitokea benchi.

Chelsea ilikuwa ikimfuatilia kwa makini nyota huyo wa Kimataifa wa Ufaransa, ambaye alifunga mabao kumi msimu uliopita licha ya kuwa alipewa dakika chache, lakini ikakataliwa.



Spurs pia ilionekana kukataliwa baada ya kukataa ada ya euro milioni 60 na Bayern na wawakilishi wake kukataa uhamisho wa kudumu.

Lakini pande hizo mbili zilifikia azimio la kushtukiza Jumatatu usiku, na Tel kukataa ofa kutoka kwa Arsenal, Aston Villa na Man United kusaini mkataba wa mkopo wa miezi sita na Tottenham.

Licha ya hapo awali kudhaniwa kuwa mkopo wa moja kwa moja, Spurs inaripotiwa kupata chaguo la kumnunua Tel msimu wa majira ya joto kwa ada ya kati ya euro milioni 55 hadi 60.

HABARI MICHEZO

## Fadlu: Simba ugenini kama nyumbani

INATOKA UKURASA 24

Michezo Nipashe (KTDMN), Simba imeshinda mechi za ugenini dhidi ya Azam FC mabao 2-0, bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, Prisons, Mashujaa FC, Pamba Jiji na Singida Black Stars, 5-2 dhidi ya Kagera Sugar, na 3-0 dhidi ya Tabora United.



Fadlu aliwashukuru mashabiki wa soka mkoani Tabora, akiwataka na wa Manyara kufanya kama walivyofanya wenzao ili wawape zawadi ya ushindi.

"Nadhani hata Manyara itakuwa kama Tabora, ningeomba iwe zaidi, na sisi tutawapa zawadi ya ushindi kwani tumedhamiria kwenda kuchukua pointi tatu zingine," alisema Fadlu.

Wakati huo huo, Daktari wa Simba, Edwin Kagoba, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa klabu hiyo juu ya afya ya Kibu Denis, ambaye aliumia kwenye mchezo uliopita.

Alisema japo kuna wasiwasi kama atatumika au la kwenye mchezo wa kesho dhidi ya Fountain Gate, lakini hajapata majeraha ya kumweka nje ya uwanja kwa muda mrefu.

"Ni kweli mchezaji wetu Kibu alipata matatizo kwenye mguu wake wa kushoto katika mchezo dhidi ya Tabora United. Alikuwa na shida sehemu mbili, kwenye 'enka', na sehemu ya robo tatu ya chini ya mguu, hali yake kwa sasa iko vizuri, anaendelea na matibabu, yuko kwenye hatua ya pili ya matibabu, tunategemea leo (jana) au kesho (leo), atakapopita kwenye hatua zote za matibabu anaweza kuwapo kwenye mchezo wetu ujao.

"Ila hii ni nusu kwa nusu kuwapo, kuna vitu tunaviangalia leo na kesho, lakini niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba kwamba hali yake si mbaya si ya kumweka nje muda mrefu," alisema daktari huyo.

Wachezaji, benchi la ufundi na pamoja na Uongozi wa klabu hiyo, jana walilitembelea Bunge la Jamhuri ya Muungano linaloendelea na vikao vyake jijini Dodoma.

Simba iliweka kambi ya muda jijini humo, ikitokea Tabora kujiandaa na mchezo wa kesho dhidi ya Fountain Gate, mkoani Manyara.

# TSHABALALA: KWA SASA KILA MECHI KWETU NI MUHIMU

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', amesema kwa sasa wameingia mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara ambapo hawatakiwi kufanya makosa yoyote yatakayowafanya kudodosha pointi.

Tshabalala amesema kutokana na umuhimu huo, kila mchezo kwao wanauchukulia kwa umuhimu mkubwa kuhakikisha wanavuna pointi tatu.

Akizungumza na Nipashe jana muda mfupi baada ya kutoka bungeni walipoalikwa kwenda kupongezwa kwa kufika hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, alisema watahakikisha wanazidi kupambana na kuongeza umakini.

"Tumeingia mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, ni wa lala salama, kila timu inapambana kuhakikisha inafanya vizuri ili kuangalia mwisho wa mzunguko huu itakuwa kwenye nafasi gani, Simba tunalifahamu hilo, na sisi tunazidi kuongeza umakini kuhakikisha tunafanya vizuri.

"Kila mechi kwetu kwa sasa ni muhimu na tunaicheza kwa umakini mkubwa, hii ni hatua ambayo ukipoteza pointi inakugharimu sana..., kama wachezaji tutaendelea kupambana na kuhakikisha tunapata ushindi kila mchezo," alisema Zimbwe.

Baada ya juzi Simba kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 mbele ya Tabora United kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, kesho itashuka tena uwanjani kucheza na Fountain Gate mkoani Manyara.

Mpaka sasa Simba wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 43 wakifuatiwa na watani zao, Yanga wenye pointi 42 huku Azam FC wakishika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 36.




Kiungo wa Arsenal, Mwingereza, Declan Rice (kushoto), akiwania mpira na Kiungo wa Manchester City, Mreno Bernardo Silva (kulia), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates mwishoni mwa wiki na Arsenal kushinda mabao 5-1. **PICHA: MTANDAO**

# Tabora hasira sasa kwa Namungo FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba, Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, timu ya Tabora United, leo itashuka tena uwanjani hapo ikiwa na lengo la kumalizia hasira zake dhidi ya Namungo FC.

Wakati Tabora ikiuchukulia mchezo huo kuwa ni wa kutaka kuwafariji mashabiki wake kwa kipigo, Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, alisema wapinzani wao wasichukulie kuwa utakuwa mchezo rahisi kwao.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, alisema hawatokubali tena matokeo mabaya kwenye uwanja wao wa nyumbani, na hasira zote za kufungwa na Simba watazimalizia kwa Namungo.

"Matokeo mabaya dhidi ya Simba yasituvunje moyo, na wala yasitutoe kwenye reli, tunajua mzunguko wa pili hatukuuanza vizuri, lakini tunawataka mashabiki wetu waje kwa wingi uwanjani, tunawahakikishia kuwa tunafanya kila njia ili tuwafute machozi," alisema Christina.

Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, amesema maandalizi yamekamilika na wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo ambao alisema utakuwa mgumu.

"Tunakwenda kucheza na Tabora United, tunawaheshimu, ni moja ya timu nzuri sana, imeimarika kwenye kila idara, ni washindani, tunacheza nao haijalishi wametoka kufungwa na nani, japo tunajua ni ngumu kwa sababu hawatotaka kufungwa tena.

"Sisi tunaingia tukiwa na kikosi chetu ambacho kimeimarika kwa kuongeza baadhi ya wachezaji kwenye dirisha dogo, nimewaona, nadhani wataongeza kitu," alisema Mgunda.

Wakati Tabora United, ikiwa kwenye nafasi ya tano na pointi zake 25, Namungo inakamata nafasi ya 12, ikiwa na pointi 17, zote zikiwa zimecheza michezo 16.

Mechi nyingine itapigwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma, wakati wenyeji, Dodoma Jiji wakiikaribisha Pamba Jiji.

Dodoma Jiji itaingia uwanjani ikiwa nafasi ya tisa na pointi zake 19, huku Pamba Jiji ikiwa nafasi ya 14 na pointi 12 ilizovuna hadi sasa.

## *Ramovic kusaka ushindi wake wa saba Ligi Kuu*

INATOKA UKURASA 24

kusajiliwa kwake kwenye dirisha dogo.

"Tumeona bado hajawa fiti kucheza, hatuwezi kulazimisha acheze kwa haraka, anaweza kupata majeraha, taratibu tunamweka fiti na atakapokuwa tayari atatumikia timu," alisema.

Kwa upande wa Kocha wa KenGold, Omari Kapilima, alisema ana imani na kikosi chake kutokana na maboresho waliyoyafanya.

"Tumeongeza wachezaji wenye uzoefu mkubwa na Ligi Kuu, nina imani mchezo wa kesho tunaweza kupambania na kuzipata pointi tatu," alisema Kapilima.


Aliongezea kuwa hawataweza kumtumia Morrison kwa sababu ni majeruhi, anaendelea kupona.

KenGold inakutana na Yanga huku ikiwa inaburuza mkia kutokana na kujikusanyia pointi sita pekee katika michezo 16 waliyocheza, wakizidiwa ponti 36 na wapinzani wao hao waliopo kwenye nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo.

# Michezo

Jumatano Februari 5, 2025

Nipashe

UKURASA 21

**Ronaldo afikisha ushindi mechi 700 ngazi ya klabu**

# Ramovic kusaka ushindi wake wa saba Ligi Kuu

●●●Azitaka pointi tatu kwa KenGold FC iliyoboreshwa, atoa pia sababu Jonathan Ikangalombo...

**Na Faustine Feliciane**

AKIWA tayari ameiongoza timu yake kupata ushindi kwenye michezo sita mfululizo ya Ligi Kuu aliyoisimamia akiwa Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, leo ana kibarua kingine cha kusaka ushindi wa saba kwenye mchezo dhidi ya KenGold FC utakaopigwa Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Yanga inawakaribisha KenGold huku ikitoka kupata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Kagera Sugar juzi kwenye uwanja huo.

KenGold wanawakabili Yanga leo huku wakiwa na kikosi kilichoboreshwa kwa kuongezwa nguvu baada ya kufanya usajili mkubwa katika dirisha dogo la Januari, ambapo kina baadhi ya nyota wakubwa wakiwamo mchezaji wa zamani wa Yanga na Simba, Bernad Morrison na Kelvin Yondani.

Hata hivyo, taarifa za ndani zinadai Morrison anaweza akaukosa mchezo wa leo kutokana na kuwa majeruhi.

Kocha wa Yanga, Ramovic akizungumzia mchezo wa leo, jana alisema watajitahidi kutumia nafasi katika mipira itakayodondoka nyuma ya mstari wa mabeki wa wapinzani wao.

Alisema anaamini mchezo utakuwa mgumu kutokana na maboresho ya kikosi cha wapinzani wao hao, lakini lazima wapambane kupata ushindi.

"Yanga tumechukua ubingwa wa Ligi Kuu misimu mitatu mfululizo, tunataka ubingwa wa nne, sasa ili kufikia hapo ni lazima kushinda mchezo huu wa kesho (leo), tunatakiwa kupambana, kutumia vizuri nafasi tutakazozitengeneza, lakini pia kuwa na nidhamu kwenye kujilinda," alisema.

Aidha, Ramovic amegusia kuhusu mchezaji wake mpya, Jonathan Ikangalombo ambaye bado hajaanza kuichezea timu hiyo tangu

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji kinara wa mabao Yanga, Clement Mzize.

## Fadlu: Simba ugenini kama nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameonekana kukoshwa na idadi kubwa ya mashabiki wa soka wanaojitokeza mikoani, akisema imekuwa chachu ya wachezaji wake kucheza kwa kujituma na kupata ushindi kwa asilimia 100 kwenye michezo ya ugenini ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imekuwa kama ipo nyumbani.

Akizungumza jijini Dodoma jana, ambako timu hiyo imeweka kambi ya muda kabla ya kuivaa Fountain Gate, katika mechi ya raundi ya 17 ya Ligi Kuu itakayopigwa kesho, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa uliopo Babati mkoani Manyara, kocha huyo alisema ameshangazwa na idadi kubwa ya mashabiki wanavyojitokeza kwenye viwanja vya mikoani, na cha ajabu zaidi ni kwamba zaidi ya asilimia 90 wamekuwa wakiishangilia Simba kwa nguvu zote, kitu ambacho kinamfanya yeye na wachezaji wake kufanya kila juhudi kuhakikisha wanaondoka uwanjani na furaha baada ya mchezo.

"Nimeona kwenye michezo mingi mikoani, kumekuwa na mashabiki wengi uwanjani na wanakuwa wanatushangilia sisi, kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mashabiki walitia fora, walijitokeza kwa wingi zaidi, uwanja ulijaa sana, na karibuni wote walikuwa upande wetu, utagundua hilo bao linapofungwa, uwanja mzima unasimama kushangilia, tulikuwa ugenini, lakini ni kama nyumbani tu, hili pamoja na mambo mengine ya ufundi na mifumo, lakini nalo kiasi kikubwa linatusukuma sana kupata ushindi," alisema.



Simba imeshinda mechi zote nane ilizocheza ugenini mpaka sasa, ikiwa kinara wa kushinda mechi nyingi za ugenini mpaka sasa.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu za

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >